UKURASA WA 3

**Majaliwa** awashukia wanaong'oa nguzo, mabango ya anuani za makazi, kuyauza kama vyuma chakavu



UKURASA WA 3

**Watiwa** mbaroni tuhuma kughushi risiti za TRA kisha kujipatia mamilioni



UKURASA WA 11

MAISHA YALIVYO:

**Viashiria** uovu nyumba ya baba yako


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

JUMAPILI

Jumapili Februari 9, 2025 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581947

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com

MIAKA 30 Nipashe

Mwanga wa Jamii

www.ippmedia.com


RIPOTI MAALUMU

# Haya hapa mambo sita yanayogharimu maisha barabarani

• **Wenye** mabasi wafichua mzizi wa tatizo; miezi miwili watu 78 wafariki dunia... *Ukurasa 4*

UKURASA WA 24



## Yanga kicheko sare ya Simba

KLABU ya Yanga imeweka wazi kuwa imefurahia mno sare ambayo watani wao wa jadi Simba waliipata Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Tanzanite...

## Serikali yafunguka upatikanaji wa ARV, yasisitiza haziuzwi

UKURASA 3



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, wakati wa mkutano wa pamoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. Mkutano huo, pamoja na mambo mengine ulijadili hali ya ulinzi na usalama Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Wengine ni Mwenyekiti wa SADC na Rais wa Zimbabwe, Emerson Mnangagwa (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa EAC na Rais wa Kenya, William Ruto. **PICHA: IKULU**

WAKUU SADC, EAC...

UKURASA 2

# Njia sahihi kumaliza mapigano DRC ni hii


MICHEZO **SIMBA INA MATUMAINI UBINGWA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Serikali yapokea mapendekezo NEMC kuwa mamlaka

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, amesema serikali imeyapokea na inaendelea kuyafanyia kazi mapendekezo matatu ya marekebisho ya Sheria ya Mazingira Sura 191.

Miongoni mwa mapendekezo hayo ni kanuni ya kulifanya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuwa mamlaka, umuhimu wa kutunga Sheria ya Uchumi wa Buluu na kutambuliwa kisheria kwa Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni (NCMC).

Mhandisi Masauni alisema hayo juzi wakati akichangia Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa Mwaka 2024 iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jackson Kiswaga, bungeni jijini hapa.

Masauni aliipongeza kamati hiyo kwa mchango wake na kusema kuwa ni wenye maono katika kuleta mabadiliko kwenye sekta ya uhifadhi wa mazingira na kusisitiza kuwa dhamira ya Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais ni kuyafanyia kazi maoni yaliyotolewa.

"Kama ambavyo tuliwaahidi kwenye kamati, Mheshimiwa Spika naomba mbele yako niahidi tutayafanyia kazi yale yote mliyotushauri wakati wa michango ya wabunge na taarifa ya kamati. Tayari tumeandaa mpango kazi kabambe ambao mpaka sasa tunavyozungumza, hakuna hata kipengele hatujakitekeleza kama tulivyojipangia kwa hiyo tunakwenda vizuri," alisema.

Mhandisi Masauni alisema kuwa ni matamanio ya serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kuona maeneo hayo matatu yaliyoainishwa, ikiwezekana Bunge lijalo kwa ushirikiano mkubwa lipitishe.

Awali, akiwasilisha taarifa hiyo, Kiswaga alisema azimio la Bunge kuwa serikali itoe mafunzo kwa wataalamu wa ndani wawe na ujuzi wa kuandaa mapitio ya tathmini ya athari kwa mazingira limetekelezwa kikamilifu. Kiswaga ambaye pia ni Mbunge wa Kalenga (CCM), alisema Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha Februari hadi Desemba 2024 imetoa mafunzo hayo kwa watumishi 75.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akibonyeza kitufe kuzindua utoaji wa huduma za barua za utambulisho kwa njia ya kidijitali na utoaji wa vishikwambi wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Anwani za Makazi, jijini Dodoma, jana. Kulia ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar, Nadir Abdulatiff Awady. **PICHA: OWM**

MKUTANO WA DHARURA DAR

# Wakuu SADC, EAC: Njia sahihi kumaliza mapigano DRC ni hii

**Na Jenifer Gilla**

VIONGOZI wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wamesema njia sahihi ya kumaliza mgogoro mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ni kukaa meza moja na kuzungumza na si visasi.

Wamesisitiza mazungumzo, ushirikiano na ulinzi wa maisha ya raia, viwe msingi wa hatua zote zitakazochukuliwa katika kuleta amani katika nchi hiyo.

Wakuu hao wamekutana kwa dharura jijini Dar es Salaam baada ya kundi la waasi wa M23 kuanzisha mapigano mapya mashariki mwa DRC.

Kundi hilo limeuteka Mji wa Nyabibwe ulioko katika ukingo wa Ziwa Kivu, Jimbo la Kivu Kusini nchini DRC kwa madai ya kujihami na mashambulizi ya Jeshi la Serikali ya DRC.

Akizungumza katika mkutano wa dharura jana jijini Dar es Salaam uliolenga kujadili mgogoro huo wa DRC ili kutafuta suluhisho la kudumu na kurudisha amani katika nchi hiyo, Rais wa Kenya, William Rutto ambaye pia ni Mwenyekiti wa EAC, alisema:

"Ili kupatikana suluhu ya haraka na kudumu katika mgogoro unaoendelea mashariki kwa DRC, ni muhimu pande zinazopigana kusitisha mapigano na kuzungumza."

Alisema ili hilo litokee ni muhimu mapigano nchini Kongo yasitishwe ili kuunda mazingira yatakayowezesha mazungumzo ya kujenga na utekelezaji makubaliano ya kina ya amani.

Hivyo, Rais Ruto aliyahimiza makundi yote yenye silaha nchini DRC, wakiwamo M23, kusitisha mashambulizi kwa jeshi la DRC ili kuepuka hatua za kulipiza kisasi zitakazokwamisha juhudi kusitisha mapigano kwa haraka.

"Ni lazima tuwahimize wadau wote waachane na tofauti zao na kushiriki katika mazungumzo yenye tija kwa lengo la kupata suluhisho la kudumu kwa kushughulikia mizizi ya mgogoro huu," alisema Ruto.

Alisisitiza kujifunza kutoka kwa mchakato wa amani wa Rwanda na Nairobi na kuhimiza mtazamo wa pamoja wa kikanda katika kushughulikia mgogoro huo.

Alitoa wito kwa nchi wanachama kuongeza juhudi zao kuhakikisha kunapatikana suluhisho litakalohakikisha nchi hiyo inakuwa na amani na utulivu wa kudumu.

"Hii ni fursa ya kihistoria kwetu, kama majirani wa DRC, kuhamasisha nia yetu ya pamoja kuwa mpango mmoja wenye mshikamano, mbinu ya kugawanyika itaathiri maendeleo yetu," aliongeza.

Rais Ruto alimshukuru Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo na kupongeza juhudi za EAC na SADC kwa kuonesha uharaka katika kushughulikia hali mbaya ya usalama na kibinadamu nchini DRC.

Rais wa Zimbabwe na Mwenyekiti wa SADC, Emmerson Mnangagwa, alitoa wito kuwapo mpango madhubuti wa kutatua mgogoro huo, akiwasisitiza viongozi wa kikanda hatowaangusha wananchi wao.

Alisema SADC itaendelea kushiriki kikamilifu kuhakikisha suluhu inapatikana kwa njia ya amani mashariki mwa Kongo.

"Hatupaswi kuwaangusha watu wa kanda zetu. Wanatuamini sisi. SADC itaendelea kushiriki kikamilifu kuhakikisha amani inapatikana," alisema Mnangagwa.

Aliongeza kuwa hali ya machafuko mashariki mwa DRC ina athari kubwa kwa bara zima, hivyo mataifa ya Afrika yanapaswa kushikamana kama walivyofanya wakati wa harakati za ukombozi.

"Hatua zetu lazima ziwe za pamoja na ziimarishwe ili kuhakikisha tunafanikisha lengo letu kuu: amani ya kudumu kwa watu wa DRC," alisema.

Mnangagwa pia alitoa pole kwa familia za wanajeshi na walinda amani waliopoteza maisha yao katika mgogoro huo na kuwa anatambua mateso makubwa wanayopitia raia wema nchi hiyo.

Rais Samia alisisitiza Tanzania imedhamiria kusaidia juhudi za kuimarisha amani na usalama katika eneo hilo.

"Tuna jukumu la pamoja la kushughulikia changamoto za usalama ambazo zimeathiri vibaya maisha ya raia wasio na hatia.

"Mkutano huu ni fursa ya kujitathmini na kujipanga upya katika kuhakikisha tunaleta amani na uthabiti wa kudumu," alisema.

Alitoa wito kwa pande zote zinazohusika katika mgogoro wa DRC kushiriki mazungumzo kwa nia njema na kuweka mbele maslahi ya wananchi wa Kongo.

"Lazima tushirikiane kwa dhati kutafuta suluhisho jumuishi na la kudumu ambalo litahakikisha watu wa DRC wanapata amani waliyokuwa wakiitamani kwa miongo kadhaa," alihitimisha.

Mkutano huo uliangazia haja ya jamii ya kimataifa kuunga mkono juhudi za kikanda kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji makubaliano ya amani.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

## Serikali yafunguka upatikanaji ARV, yasisitiza kuwa haziuzwi

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya imetoa ufafanuzi kuhusu upatikanaji dawa za kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI (ARV), ikieleza kuwa zipo za kutosha na haziuzwi.

Jana, Nipashe iliripoti kuhusu madai ya baadhi watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) wanaotumia dawa hizo, wakieleza kwamba wametaarifiwa wataanza kuzinunua hivi karibuni.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Afya, Roida Andusamile, ilifafanua kuwa mikakati ya serikali ni kuendelea kuwahudumia WAVIU kama kawaida.

"Serikali kupitia wizara inaendelea kuweka mikakati thabiti na stahiki, ili kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kama kawaida.

"Watumiaji dawa hizi, hawana sababu ya kuwa na wasiwasi kuhusu upatikanaji dawa hizo," alisema.

Alisema hakuna uhaba wa ARV na kwamba wananchi hawapaswi kuwa na hofu kwa kuwa serikali itaendelea kuwahudumia kama kawaida.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya, inapenda kuwahakikishia wananchi kuwa dawa za kufubaza (kupunguza) makali ya Virusi vya UKIMWI haziuzwi na kwamba zipo za kutosha," alisisitiza.

Alifafanua kwamba wananchi wanapaswa kuendelea kutumia dawa kwa usahihi kama wanavyoelekezwa na wataalamu wa afya, ili kuzuia usugu wa vimelea vya ugonjwa huo dhidi ya dawa.

Juzi, Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA), kupitia Eva Philipo, liliiambia Nipashe kwamba kwa sasa ARV zinatolewa bila malipo, lakini wametaarifiwa kuwa zitaanza kuuzwa, japokuwa hawajaelezwa ni lini utekelezaji wake utaanza.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Majaliwa awashukia wanaong'oa mabango, nguzo anuani za makazi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amekemea tabia ya baadhi ya wananchi wasio waaminifu wanaong'oa mabango na nguzo za anwani za makazi na kwenda kuuza.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati wa kilele cha Wiki ya Anwani za Makazi sambamba na kuzindua matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi.

Alisema ni muhimu wananchi kutunza na kuwa walinzi wa miundombini ya anwani za makazi kwenye maeneo yao kwa kuwa serikali imetumia gharama kubwa katika kugharamia uwekaji huo.

"Vibao tulivyoviweka kuonesha mitaa na barabara, tunao Watanzania ambao si waaminifu wanang'oa mabago hayo na kwenda kuyauza, ni muhimu kila mmoja kuwa mlinzi wa miundombinu hiyo kwa sababu ina manufaa," aliagiza.

Waziri Mkuu alisema suala la anwani za makazi ni moja ya yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa 2021/2022- 2025/2026, ambao umeweka bayana azma ya serikali ya kujenga mfumo wa anwani za makazi na postikodi katika kata zote nchini. "Siku kama ya leo, Rais Samia alizindua utekelezaji mfumo wa anwani za makazi nchini kwa njia ya operesheni. Operesheni hiyo ilifanyika kwa muda wa miezi minne na kuwezesha ukusanyaji taarifa milioni 12.3 za anwani za makazi zilizohifadhiwa katika mfumo wa kidijitali wa anwani za makazi unaojulikana kwa jina la National Physical Addressing (NaPA)," alisema.

Alibainisha kuwa kupitia programu ya NaPA, mwananchi akiwa eneo lolote nchini na hajui sehemu ya kupata huduma za kijamii kama vile kituo cha afya au mgahawa, anaweza kutumia programu hiyo kutafuta sehemu za karibu.

"Hii ni programu bora na inarahisisha kupata huduma husika sambamba na kwenda na kasi ya kimaendeleo katika uchumi wa sasa wa kijiditali," alisisitiza.

Alifafanua kuwa mfumo wa anwani za makazi utasaidia kuchochea ukuaji wa uchumi, kuharakisha upatikanaji huduma za kijamii, kuimarisha masuala ya ulinzi na usalama, kuwezesha biashara mtandao kufanyika kwa ufanisi na kuimarisha uwezo wa kukabiliana na majanga.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, alisema wizara hiyo inaendelea kusimamia na kuendeleza miundombinu na mifumo ya msingi ambayo ni mhimili muhimu wa uchumi wa kidijitali ulioainishwa katika Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Miaka 10 (2024-2034).

Alisema mifumo hiyo inajumuisha mifumo ya utambuzi wa watu, biashara, ardhi na makazi. "Katika muktadha huu, utekelezaji Mfumo wa Anwani za Makazi ni hatua ya kimapinduzi inayolenga kuboresha utambuzi na utoaji huduma kwa wananchi nchini," alisema.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Nadir Abdulatiff Awady, alisema uwekaji anwani za makazi kwa upande wa Zanzibar umekamilika kwa asilimia 100. Hivi sasa wanaendelea kuwahamasisha wananchi matumizi ya anwani hizo.

Awali Naibu wa Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema kabla ya utekelezaji mfumo huo, ilikuwa ni vigumu kwa mgeni kufika katika baadhi ya maeneo ila kwa sasa imerahisishwa baada ya utekelezaji mpango huo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema Jiji la Dodoma limetenga Sh. milioni 300 kwa ajili ya kuweka kamera za CCTV katika barabara kwa ajili ya kuimarisha usalama na kuzuia wizi wa miundombinu.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Stephen Wassira (kulia), akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Tarime, mkoani Mara, jana. **PICHA: CCM**

# Mbaroni kwa tuhuma za kughushi risiti za TRA, kujipatia mamilioni

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watu wawili ambao majina yao yamehifadhiwa, kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kughushi risiti za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Kamanda wa Polisi mkoani Ruvuma, Marco Chilya, alisema kupitia vitendo hivyo, watuhumiwa hao wamejipatia zaidi ya Sh. milioni 57 .8 kutoka kwa baadhi ya wafanyabiashara katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Alisema kuwa Februari Aprili Mosi mwaka huu, askari polisi kupitia Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai waliwakamata watuhumiwa hao kwa madai ya kujihusisha na kughushi risiti za TRA kwa kujipatia ujira jumla ya risiti 25 zenye thamani fedha hizo.

Kamanda Chilya alisema watuhumiwa hao wanaendelea kuhojiwa na polisi kwa lengo la kubaini mtandao wote unaojihusisha na kuwadanganya wafanyabiashara kwa kughushi kwa kutumia nembo ya TRA kutengeneza risiti bandia zikiwamo ada za shule za msingi na sekondari.

Kamanda huyo aliwakumbusha wafanyabiashara wote mkoani Ruvuma kuhakikisha wanapofanya biashara zao, watoe risiti kwa wateja wao zenye thamani halisi ya bidhaa wanazoziuza na kuwa makini kwa wale wanaowagushi.

Wakati huo, Esta Mapunda (48), mkazi wa Kijiji cha Ng'ombo, Kata ya Chiwanda, Wilaya ya Nyasa, amefariki dunia baada ya kukamatwa na mamba kisha kuzama naye majini Ziwa Nyasa.

Vilevile, Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kupatikana na nyara za serikali kupitia operesheni na msako unaoendelea kufanyika kwa kushirikina na askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

Alisema kuwa wilayani Tunduru wamewekamata watuhumiwa Godfrey Mbunda (51) na Hamis Komba (42), wote wakazi wa Kijiji cha Fundimbanga, wakiwa na meno manane ya tembo na vipande vinne vya meno ya tembo yenye uzito wa kilo 515, vilivyohifadhiwa katika mfuko wa sandarusi na kufunikwa turubai.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Haya hapa mambo sita yanayogharimu maisha barabarani

## -Wenye mabasi wafichua mzizi wa tatizo; miezi miwili watu 78 wafariki dunia...

**Na Restuta James**

TAARIFA zilizoripotiwa na vyombo vya habari kati ya mwezi Desemba 2024 na Januari 2025, zinaonesha kwamba watu 78 wamepoteza maisha kwa ajali za magari katika kipindi cha siku 62.

Hii ni sawa na wastani wa watu wawili hufariki dunia kwa siku, vyanzo vikuu vikiwa ni mwendokasi, matumizi ya vilevi na matatizo ya kiufundi.

Vingine ni uzembe wa madereva, kutozingatia Sheria ya Usalama Barabarani na miundombinu mibovu, hasa mashimo barabarani.

Kwa Desemba pekee, ajali 10 ziliripotiwa na vyombo vya habari, zikisababisha vifo vya watu 61 na Januari zilikuwa ajali nne zilizogharimu maisha ya watu 17.

Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), hakiko nyuma katika kufuatilia kinachojiri barabarani. Kimetoa mapendekezo manne kinayoamini yatapunguza ajali za barabarani.

Wamependekeza kuweka njia za mchepuko kila baada ya kilometa 50 na kurekebisha mitaala kwa ajili ya kuzalisha madereva wenye sifa stahiki.

Katika mazungumzo na Nipashe Jumapili, Katibu Mkuu wa TABOA, John Priscus anasema ajali nyingi zinasababishwa na makosa ya kibinadamu na ubovu wa miundombinu.

Anasema kwa ajali zinazotokea kutokana na hitilafu ya magari, zinaweza kuzuilika kama kutakuwa na eneo la kuchepusha gari pindi hitilafu inapotokea, badala ya kuliacha barabarani, jambo linalosababisha gari lingine kuligonga.

"Sehemu ambazo ajali zinatokea zinajulikana, kwenye kona kali, mashimo barabarani na milima, unakuta madereva wanapata ajali kwa sababu ya kukwepa shimo, mashimo yanasababisha 'spring' kukatika na kusababisha gari kukosa mwelekeo," anasema.

Priscus anaendelea kueleza: "Tumeshauri mara kadhaa kwamba kwenye kona na milima, kuwekwe escape route (michepuko), ili gari linapopata dharura liegeshe pembeni.

"Wanatengeneza barabara kama vile magari hayatapata dharura. Unakuta kilometa nyingi hakuna sehemu ya kuchepuka, ili gari likipata dharura litoke nje ya barabara ili lisisababishe ajali kwa magari mengine.

"Magari yanapopata dharura haitokei ghafla, kunakuwa na ishara. Ilipaswa dereva apate sehemu ya kusimama kwenye 'escape route' ili arekebishe, lakini hakuna.

"Matokeo yake anasimama barabarani, gari lingine linakuja kwa kasi, linagonga kwa nyuma au linalikwepa na kugongana uso kwa uso na gari lingine.

"Tumeomba wafanye mchepuko hata kwa kiwango cha changarawe kama lami ni gharama. Kama barabara ya Morogoro ni changamoto. Kwenye milima yote tumeshauri ipanuliwe. Ajali zinapoteza maisha ya watu na ni hasara kubwa kwa taifa."



Katibu Mkuu wa TABOA, John Priscus. **PICHA: MTANDAO**

Katika hilo, kiongozi huyo wa TABOA anashauri serikali kuweka mchepuko kila baada ya kilometa 50 kwenye barabara zote kuu (highways).

"Mabasi yote yamefungwa GPS, yanafuatiliwa mwendo, ndio maana ninasema ajali nyingi sisi tunasababishiwa. Huwezi kuwa unabana upande mmoja wa mabasi, halafu unaachia magari madogo.

"Tunashauri magari madogo yaangaliwe utoaji leseni na jeshi la polisi lifanye ukaguzi wa haya magari mengine kama linavyofanya kwenye malori na mabasi," anasema.

Priscus anasema udhibiti unaofanywa kwa madereva na wamiliki wa mabasi, unapaswa kutolewa pia kwa magari madogo ya watu binafsi.

Anasema hilo litawezekana kwa kuweka mkazo kwenye mitaala ya udereva ili madereva wote wawe na leseni kubwa.

Anasema baadhi ya ajali zinazohusisha malori na mabasi dhidi ya magari madogo binafsi, mara nyingi makosa yanakuwa ya magari madogo.

Anasema madereva wa mabasi ya abiria na wale wa malori, wana mafunzo kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na wanapimwa kwa kina kabla ya kupewa leseni, jambo alilosisitiza halifanyiki kwa madereva wa magari madogo.

Mmoja wa madereva wa magari yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi (IT), ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, anasema wengi wao wanaanza safari wakiwa wamechoka na wanaendesha kwa mwendo kasi ili warudi kuchukua gari lingine.

"Unakuta mchana kutwa mtu ameshinda bandarini kutoa gari, halafu anaanza safari usiku kwenda Tunduma. Wengi wanaangalia kuwahi kufika Mbeya ili arudi kuchukua gari lingine, ndio maana baadhi wanapoteza maisha na mali (gari) husika," anasema.

Anashauri uwekwe utaratibu maalum wa kusafirisha magari hayo, ikiwamo muda sahihi wa kuyatoa bandarini na kupanga muda wa kufika kila kituo ili kupunguza mwendo kasi kwa madereva hao.

"Mfano, dereva akiondoka Dar es Salaam, atie saini kwa polisi barabarani kwamba ameondoka muda fulani na atategemewa kufika Morogoro muda fulani, ili walau atembee mwendo wa kilometa 80 hadi 100 kwa saa," anasema.

Mmoja wa madereva wa magari madogo jijini Dar es Salaam, Martin Charles, anasema ajali nyingi zinatokana na uzembe wa madereva hao, kuendesha gari bila kuzingatia alama za usalama barabarani na kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari.

"Lakini wengine unakuta mtu ameanza kuendesha gari mwezi uliopita, mwezi mmoja baadaye anataka kuendesha masafa marefu kwenda mkoani. Mkazo wa elimu ya udereva umewekwa sana kwa madereva wa malori na mabasi. Ninaona wengi wenye magari madogo hawana uzoefu wala mafunzo ya kutosha," anasema.

### WAFUNGIWA LESENI

Hivi karibuni, madereva 64 wa mabasi makubwa na madogo yanayotoa huduma za usafirishaji katika mkoa wa Kilimanjaro, wamefutiwa leseni kutokana na makosa ya mwendokasi, kusababisha ajali, ulevi na kuyapita magari mengine bila tahadhari.

Madereva hao walifungiwa leseni zao za udereva kwa kipindi cha miezi sita kwa mujibu wa Kifungu cha 28((b) cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Baadhi ya ajali katika kipindi tajwa ni pamoja na iliyotokea katika Kijiji cha Unyampiti, Kata ya Unyahati, wilayani Ikungi, mkoani Singida ikihusisha gari aina ya Toyota Alphard lenye namba za usajili T 128 EKF, mali ya Anastazia Gozbert, ambalo liligongana na lori lenye namba za usajiri T 467 EJP ikiwa na tela lake, T 439 EJN aina ya Howo, mali ya East Africa Logistic Ltd.

Ajali nyingine ilitokea eneo la Mikese, mkoani Morogoro, kwa kuhusisha gari aina ya Coaster liligongana na lori la mizigo na kusababisha vifo vya watu 15 na kujeruhi wengine saba. Baadaye mmoja wa majeruhi hao alifariki dunia wakati anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kufanya idadi ya vifo kuwa vya watu 16.

Desemba 21 mwaka jana, basi la kampuni ya Capro One lenye namba za usajili T857 DHW lilifeli breki katika mteremko na kurudi nyuma kisha kupinduka na kusababisha vifo vya watu 11 na wengine 16 kujeruhiwa.

Desemba 22 mwaka jana, ajali nyingine ilikatisha uhai wa aliyekuwa Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu Ofisi ya Msajili wa Hazina, Amos Nnko pamoja na binti yake, Maureen Nnko wilayani Same, mkoani Kilimanjaro.

Desemba 24 mwaka jana, watu saba walifariki dunia na wengine 10 kujeruhiwa kwenye ajali iliyotokea katika eneo la Michungwani, wilayani Handeni, Mkoa wa Tanga, barabara kuu ya Segera-Chalinze.

Usiku wa Desemba 25 mwaka jana, watu 11 walifariki dunia na wengine 13 kujeruhiwa, baada ya gari dogo la abiria aina ya Coaster lililokuwa linatokea Mkata kwenda Tanga mjini, kugongana na lori la mizigo aina ya Fuso, lililokuwa linatokea Lushoto kwenda Dar es Salaam.

Ajali nyingine ilitokea Desemba 25 jana ambayo ilihusisha lori la mizigo namba T 707EBZ na basi dogo aina ya Coaster T 497DZW, katika barabara ya Segera Chalinze na kusababisha vifo vya watu wanne.

Mkoani Lindi, eneo la Machole, Desemba 25 mwaka jana, ajali ilisababisha kifo cha mtu mmoja na kujeruhi watu saba.

Desemba 28 mwaka jana, watu sita wakiwamo mume na mke pamoja na walimu wanne wa shule moja, walifariki dunia mkoani Ruvuma katika kijiji cha Buluma, wilayani Mbinga barabara ya Mbinga-Mbambabay, eneo la kona za Chunya, baada ya gari aina ya Prado T647 CVR walilokuwa wanasafiria, kugonga gema na kuwaka moto.

Wakati hali ikiwa hivyo Desemba, Januari 10 mwaka huu, gari la abiria maarufu daladala liligonga magari matatu katika eneo la Iseni, Kata ya Butimba, wilaya ya Nyamagana na kusababisha kifo cha mtu mmoja.

Ajali nyingine ilitokea katika Kijiji cha Mazizi, Msoga mkoani Pwani, ikihusisha gari la abiria aina ya Coaster lililogonga lori kwa nyuma na kusababisha kifo cha mtu mmoja.

Nyingine ni iliyotokea Kata ya Segera, wilaya ya Handeni mkoani Tanga na kusababisha vifo vya watu 11, baada ya kugongwa na lori lililokuwa limebeba saruji, lilipoteza uelekeo.

Nyingine ni ya waombolezaji wanne waliokuwa wanasafirisha mwili wa marehemu kutoka Dar es Salaam kwenda Bukoba, Mkoa wa Kagera waliopoteza maisha katika eneo la Msolwa.

### SALAMU ZA RAIS

Katika salamu zake za mwaka mpya, Desemba 31, 2024, Samia Suluhu Hassan, alisema takwimu za Jeshi la Polisi Tanzania zinaonesha kati ya Januari hadi Desemba mwaka jana, kulitokea ajali 1,735, kati ya hizo 1,198 zilisababisha vifo vya watu 1,715, wengine 2,719 wakijeruhiwa.

Alisema asilimia 97 ya ajali hizo zilitokana na makosa ya kibinadamu, hasa uzembe wa madereva. Aliagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi kuongeza mikakati ya kuzuia ajali zinazosababishwa na uzembe.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

MAKALA

# DED alipowakaribisha wananchi wamhoji matumizi ya kodi zao

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, Khamis Katimba amewakaribisha wananchi kufika ofisini kwake kuhoji matumizi ya fedha zinazokusanywa na kutumiwa na halmashauri hiyo.

Ni rai aliyotoa mwanzoni mwa mwaka huu wakati wa kikao cha wadau wa maendeleo katika ukumbi wa halmashauri hiyo, akisisitiza kuwa kila fedha inayokusanywa na kutumika ina maelezo yake.

Katimba alitoa kauli hiyo baada ya Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Sebastian Waryuba kumshauri kuwaeleza wananchi matumizi ya fedha zinazokusanywa na halmashauri hiyo.

Waryuba alianza kwa kumsifu mkurugenzi huyo kwa kuongeza mapato, hata kufikia asilimia 82 ya lengo la kukusanya mapato ya ndani, katika kipindi cha miezi sita pekee (Julai - Desemba 2024).

"Nimefurahi kushuhudia kasi hii ya ukusanyaji mapato bila kutoana damu, mabadiliko haya yanaonesha kwamba huko tuendako tutafika salama.

"Mkurugenzi kasi hii isipungue, umeaminiwa na sisi tunakuamini kwa mikakati yako, simama imara na makusanyo yetu yapande zaidi lakini waone na matumizi yake," alisema Waryuba.

Akitoa ufafanuzi wa kauli hiyo ya Waryuba, Mkurugenzi Katimba alisema wananchi wakiona fedha zao zinafanya kazi gani, watahamasishana kulipa kodi kwa hiari.

"Mimi ninawaahidi, wao kazi yao ni kulipa kodi halafu waje waniwajibishe kwa matumizi ya fedha zao. Ninawaomba waendelee kulipa kodi ya serikali, lakini waje kuniwajibisha kwa matumizi ya fedha zao.

"Ofisi yangu ipo wazi kwa wote, hata akija mmoja mmoja ninaruhusu aje ofisini kwangu, aje aniulize 'umekusanya shilingi ngapi na umetumia shilingi ngapi?' Nitamueleza. Ofisi ipo wazi, ni ofisi ya wananchi wote, sisi ni dhamana tu," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, Pius Mwelase alisema halmashauri hiyo ilikuwa haijawahi kukusanya mapato ya ndani asilimia 82 katika kipindi cha miezi sita pekee.

"Haijawahi kutokea mpaka Desemba kukusanya asilimia 82 kwenye halmashauri yetu, viporo vyote toka halmashauri yetu ianze tunavimaliza na kama kuna vingine semeni, sasa pesa ipo.

"Ubunifu aliokuja nao mkurugenzi wetu umeleta mabadiliko makubwa mno, tunajivunia na tunaamini bado tuna muda wa kutosha wa kukusanya fedha zingine nyingi kutokana na mikakati iliyopo kwa sasa," alisema.

Kimsingi, Mkurugenzi Mtendaji Waryuba na wengineo nchini, wanapaswa kuwa na utaratibu maalumu wa kuwaeleza wananchi mapato na matumizi ya fedha zinazokusanywa na halmashauri zao.

Utayari wa Mkurugenzi Waryuba kuwakaribisha ofisini wananchi na kuwaeleza namna halmashauri inavyotumia kodi zao ni jambo jema, lakini halmashauri inapaswa kuwa na utaratibu maalumu wa kutoa taarifa za mapato na matumizi walau kila baada ya robo mwaka na taarifa hizo ziwe wazi kwa wananchi wote, siyo tu kwa wanaofika ofisi za halmashauri yao.

Kwa kutangaza mapato na matumizi, mfano kupitia tovuti rasmi ya kila halmashauri, ninaamini kutaongeza uwazi na uwajibikaji wa watendaji wa serikali katika fedha za umma.




Taarifa rasmi za kiserikali zinaonesha kupotea mabilioni ya shilingi ambayo yangetumika kuboresha miundombinu nchini.

Mtazamo huo wa fedha za umma kufanyiwa ubadhirifu, hata kusababisha pengo la ufanisi kwenye huduma za umma, unawasilishwa kupitia Uchambuzi wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23 uliofanywa na taasisi ya WAJIBU.

Taasisi hiyo inayosimamiwa na CAG mstaafu Ludovick Utouh, mwanazuoni wa uhasibu, imebaini miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma, inayofikia Sh. trilioni 11.857 ndani ya miaka minne (2019/20 - 2022/23).

Kiasi hicho kama kingeelekezwa kutatua uhaba wa miundombinu shuleni, kwa mfano, kingetosha kujenga vyumba vya madarasa mapya 592,850.

| Taasisi | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | Bil 560.19/- | Bil 1,781.77/- | Bil 770.91/- | Bil 676.66/- |
| S/Mitaa | Bil 863.85/- | Bil 1,400.6/- | Bil 297.86/- | Bil 499.96/- |
| Mashirika | Bil 346.8/- | Bil 1,408.36/- | Bil 2,015.78/- | Bil 1,234.67/- |
| Jumla | Bil 1,770.84/- | Bil 4,590.73/- | Bil 3,084,55/- | Bil 2,411.29 |

**Mwenendo wa viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23. CHANZO: Ripoti ya Uwajibikaji ya taasisi ya WAJIBU. Uk. 4**

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), chumba kimoja cha darasa kinajengwa kwa Sh. milioni 20 kikiwa na samani zake zote.

Akizungumza mwenendo wa makusanyo katika wasilisho lake, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Richard Sanga alisema kuwa mpaka kukamilika kwa mwaka wa fedha 2023/24, halmashauri hiyo ilikusudia kukusanya Sh. bilioni 22.338 lakini ilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 20.445.

Alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/25, halmashauri hiyo iliidhinisha Sh. bilioni 26.790, mapato ya ndani yakiwa ni Sh. bilioni 4.334 na mpaka sasa - kwa miezi sita - mapato ya ndani, zimekusanywa Sh. bilioni 3.567.

Wakizungumza kwenye mjadala wa Rasimu ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Halmashauri hiyo kwa kipindi cha 2025/26, wadau wamegusia maeneo kadhaa wakitaka yafanyiwe kazi.

Mwananchi Omari Jumanne anasema halmashauri inapaswa kuandaa mpango madhubuti kuhakikisha wafugaji wanafuga kisasa na kuachana na ufugaji wa samaki wa kizamani.

"Samaki wanalipa hapa kwetu Malinyi, halmashauri isaidie sasa namna ya ufugaji kisasa, hili litasaidia kuongeza mapato," anasema.

Mwananchi mwingine Milard Ngapulile anashauri halmashauri kuandaa mfumo mzuri wa motisha kwa walimu na hata kulipa walimu wanaojitolea.

"Halmashauri itenge fedha kwa ajili ya walimu wanaojitolea na si kuwaachia mzigo huo walimu wakuu. Pia halmashauri inapaswa kuongeza motisha kwa walimu," anasema.

Neema Mgalagala anashauri kuwapo minada ya nyama choma ili wananchi wakajiliwaze baada ya kutafuta pesa.

"Tunatafuta fedha lakini hakuna pa kuzitumia, kwanini na sisi tusiwe na mnada wa mbuzi tukajipumzishe, tunahitaji kujiliwaza kwa kula vitu vizuri," anasema.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali inastahili pongezi bwawa la Kidunda, kasi zaidi inahitajika

**SERIKALI** kupitia Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira imekuwa ikifanya kila jitihada kuhakikisha wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Katika kusisitiza hilo, serikali ya awamu ya sita imeibuka na kaulimbiu ya kumtua mama ndoo kichwani.

Kaulimbiu hiyo iliyobuniwa na Rais Samia Suhulu Hassan, inatokana na ukweli kwamba mwanamke ndiye mhusika mkuu katika suala zima la kuhakikisha maji yanapatikana katika familia kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Kutokana na upungufu wa maji katika maeneo mbalimbali, wanawake huamka mapema alfajiri kwa ajili ya kutafuta maji ambayo hupatikana kwa umbali mrefu.

Wakati wa harakati za kusaka huduma hiyo, wanawake wamekuwa wakitoa simulizi mbalimbali kuhusu majanga yanayowakabili kama baadhi yao kupoteza maisha kwa kushambuliwa na wanyama wakali na wengine kufanyiwa vitendo vya kinyama kama vile kubakwa. Baadhi yao pia wamekuwa wakidai kuwa ndoa zao ziko hatarini kuvunjika kwa kuwa wamekuwa wakitumia muda mwingi kutafuta maji huku wenza wao wakidhani kwamba wanakuwa na uhusiano na wanaume wengine.

Hiyo ndiyo hali halisi ndiyo maana Rais Samia aliamua kuibuka na kauli hiyo ili kuwaokoa wanawake na madhila yanayowakumba.

Kwa ujumla, hali hiyo pia imesababisha wanawake kutumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za uzalishaji. Kimsingi, mwanamke anabeba dhima kubwa katika familia kwa kuwa ndiyo mhimili mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Dar es Salaam ni moja ya maeneo yanayokumbwa na shida ya maji mara kwa mara hatua ambayo imeifanya serikali kuelekeza nguvu nyingi kuhakikisha huduma hiyo inapatikana. Katika kufanya hivyo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali zikiwamo uchimbaji wa visima virefu katika sehemu mbalimbali kama Kigamboni.

Hatua hiyo ni moja ya juhudi za kuongeza upatikanaji wa huduma na kuepuka utegemezi wa mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini ambayo uzalishaji wake unatokana na maji kutoka mto Ruvu ambao wakati mwingine hupungua kina nyakati za kiangazi.

Hivi karibuni, mamlaka hiyo ilialika wadau mbalimbali kwenda kushuhudia maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Kidunda, lililoko Morogoro ambalo baada ya kukamilika kwake, linatarajiwa kuhifadhi lita bilioni 190. Kukamilika kwa mradi huo ambao umekuwa katika mipango ya maendeleo tangu Tanzania ilipopata Uhuru mwaka 1961, unatekelezwa kwa pesa za ndani na utapunguza kwa kiasi kikubwa upungufu wa maji mkoani Dar es Salaam, Morogoro na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani ambayo yanahudumiwa na DAWASA. Kwa sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 27.


Kwa mujibu wa taarifa ya DAWASA, mradi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 336 hadi kukamilika kwake unalenga kuhakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika kwa wakazi wa mikoa hiyo ifikapo Desemba 2026 utakapokamilika sambamba na kutoa maji ya uhakika, mradi huo unatarajiwa kuwa suluhisho la muda mrefu kwa uhifadhi wa mazingira na maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika mikoa inayonufaika.

Kwa utekelezaji huo, serikali inastahili pongezi za dhati kwa kuwa imeonesha kwa vitendo kwamba ina dhamira ya kweli katika kuhakikisha wananchi wake wanaondokana na adha ya kukosa huduma hiyo ambayo imekuwapo kwa muda mrefu.

Pamoja na pongezi hizo, ahadi ya kwamba mradi huo utakamilika katika muda uliopangwa inapaswa kutekelezwa ili kuwapa kicheko wananchi ya kupata maji kwa uhakika badala ya hali ilivyo sasa ambapo kuna tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Mbinu hii mbadala wa pombe za viroba idhibitiwe

Na Sabato Kasika

**MWANZONI** mwa mwaka 2017, serikali ilipiga marufuku matumizi ya pakiti za plastiki kufungashiwa pombe kali maarufu kama 'viroba' kwa lengo la kulinda vijana walioko shuleni na maeneo mengine.

Serikali ilichukua hatua hiyo baada ya kubaini kuwapo kwa vijana wanaotumia pombe hizo zisizopimwa kihalali zinazowekwa katika viroba na kudhoofisha afya za wanywaji.

Licha ya kwamba umri wa mtu kuweza kunywa pombe ni miaka 18, ilibanika kuwa watoto wadogo tayari wameonekana kuwa ni wenye kuathirika na utumiaji viroba kutokana na urahisi wa upatikanaji wake.

Marufuku iliyopigwa na serikali dhidi ya pombe hizo, imezaa matunda kwa maana ya kwamba tangu wakati huo hakuna tena pombe iliyowekwa katika viroba inayouzwa katika maeneo mbalimbali.

Ikumbukwe kuwa marufuku hiyo pia ililenga kuwanusuru madereva wa bodaboda na bajaj ambao ilibainika kuwa ni waathirika wakubwa wa pombe za viroba kutokana na unafuu wa bei yake.

Licha ya kwamba serikali imefanikiwa kudhibiti viroba hivyo, wauzaji wa pombe wamekuja na mtindo mwingine wa kuendelea kuuza pombe hizo kwa bei nafuu ili kupata wateja wao wa zamani na wapya.

Kwa sasa wauzaji wanatumia mifuniko ya chupa au vikombe kama vya kuuzia kahawa kuwapimia wanywaji pombe kali ili kila mmoja anywee kulingana na uwezo wake wa fedha mfukoni.

Mteja akitaka kipimo cha kuanzia shilingi 300 na kuendelea juu, anauziwa. Hapa inaonesha kuwa baada ya serikali kupiga marufuku pombe za viroba zilizokuwa zikiuzwa kwa bei nafuu, wauzaji nao wamekuja na mbinu ya kuendeleza biashara hiyo kwa bei nafuu.

Wateja wakubwa madereva wa bodaboda, bajaj na vijana wa vijiweni ambao si jambo la ajabu kuwakuta alfajiri wakiwa katika maeneo yanayouzwa pombe hiyo wakiendelea na ulevi.

Ni hao hao ambao wakishamaliza kunywa wanaingia barabarani kubeba abiria wakiwa wamelewa, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao na wa abiria wanaowasafirisha kwenda maeneo mbalimbali.

Mkoani Dar es Salaam, kuna baadhi ya maduka na vibanda katika vituo vya daladala, wauzaji hukesha wakiuza bidhaa mbalimbali ikiwamo pombe ya kupima ambayo wateja wake wakubwa ni madereva hao.

Katika ulevi huo, wenyewe wameupa jina kuwa 'kutoa loki', lakini wanasahau kuwa mtindo huo ni hatari kwa maisha yao kwani ulevi una athari nyingi ikiwamo kukosa umakini wawapo barabarani.

Imekuwa ikielezwa kuwa matumizi ya kilevi na kuendesha chombo cha moto ni moja ya sababu zinazoongoza kwa ajali za barabarani, hivyo, ni vyema wanaoendeleza ulevi kwa mtindo huo wa sasa wadhibitiwe.

Ninadhani si vibaya mamlaka husika ikiwamo ya leseni za vileo kufuatilia jambo hili kwa lengo la kubaini jinsi ambavyo pombe zinauzwa na athari zake kwa makundi ya vijana.

Bila kuchukua hatua za kudhibiti hali hiyo, bado vijana wengi zaidi wanaweza kuendelea kuwa katika hatari ya kupoteza maisha, hasa ikizingatiwa kuwa wengi wamejiajiri kwenye udereva wa bodaboda.

Ili kudhibiti ajali za barabarani zinazohusisha madereva wa bodaboda, Jeshi la Polisi lilibuni mbinu ya kukabiliana na ajali hizo ikiwamo kila dereva kuwa na leseni ya biashara ili kutambulika kisheria.

Hatua hiyo ilichukuliwa kutokana na kuongezeka kwa ajali za barabarani, huku Taasisi ya Tiba na Mifupa, Upasuaji na Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), inapokea takriban majeruhi wa ajali 700 za barabarani kwa mwezi, asilimia 60 ya ajali zikiwa ni bodaboda.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Nguvu na mtaji wa CCM ni Watanzania



Pascal Mayalla

LEO naendelea na sehemu ya pili na ya mwisho kuhusu Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kuna wengi hawaijui nguvu ya CCM inatoka wapi, mtaji wa ushindi wa CCM mwaka hadi mwaka ni mtaji gani? Pia nitazungumzia kidogo mamlaka ya Mkutano Mkuu wa CCM kwa mujibu wa Katiba yake.

Nguvu kuu ya CCM ni wanachama wake. Hawa ndio wenye chama na ndio wenye mamlaka ya mwisho kupitia Mkutano Mkuu wa CCM. Mwanachama wa CCM, ni raia yeyote wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18. Anaweza kuwa mwanachama iwapo anakubali Imani, Malengo na Madhumuni ya CCM.

Mtu atakayekubaliwa kuingia katika CCM au kuendelea kuwa mwanachama, ni yule anayetimiza masharti ya kuwa mtu anayeheshimu watu, mtu anayefanya juhudi ya kuielewa, kuieleza, kuitetea na kuitekeleza Itikadi na Siasa ya CCM. Ni mtu mwenye kuamini kuwa kazi ni kipimo cha utu, na kuitekeleza imani hiyo kwa vitendo.

Sifa nyingine za mwana CCM ni mtu anayependa kushirikiana na wenzake, mtu ambaye siku zote yuko mstari wa mbele katika utekelezaji wa mambo yote ya umma, kulingana na miongozo ya CCM. Huwa wakati wote ni mfano wa tabia nzuri kwa vitendo vyake na kauli yake, kuwa mwaminifu na kutokuwa mlevi au mzururaji na kuwa ama mkulima, mfanyakazi au mwenye shughuli nyingine yoyote halali ya kujitegemea

Mwanachama yoyote atakuwa na haki ya kushiriki katika shughuli zote za CCM kwa kufuata utaratibu uliowekwa, haki ya kuhudhuria na kutoa maoni yake katika mikutano ya CCM pale ambapo anahusika kwa mujibu wa Katiba, haki ya kuomba kuchaguliwa kuwa Kiongozi wa CCM na ya kuchagua viongozi wake wa CCM kwa mujibu wa Katiba.

Hakuna haki bila wajibu. Wajibu wa mwanachama ni kujua kwamba Chama Cha Mapinduzi ndicho chenye nguvu, uwezo na kwamba nguvu hizo zinatokana na umoja wa wanachama, fikra sahihi za CCM na kukubalika kwake na umma. Kwa hiyo, kulinda na kuendeleza mambo hayo ni wajibu wa kwanza wa kila Mwanachama.

Mwanachama pia ana wajibu kutumikia nchi yake na watu wake wote kwa kutekeleza wajibu wake bila hofu, chuki wala upendeleo wa nafsi yake, rafiki au jamaa. Kujitolea nafsi yake kuondosha umasikini, ujinga, maradhi na dhuluma, na kwa jumla kushirikiana na wenzake wote katika kujenga nchi yake. Pia huwa wakati wote mkweli, mwaminifu na raia mwema wa Tanzania. Wajibu na sifa nyingine ni kuwa tayari kujikosoa na kukosolewa ili kuweza kuwa na msimamo sahihi wa siasa ya CCM

**KIONGOZI WA CCM**

Kiongozi wa CCM ni kila Mwanachama mwenye dhamana yoyote katika CCM aliyechaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa Katiba. Kiongozi sharti awe mtu aliyetosheka na asiwe mtu aliyetawaliwa na tamaa, awe mtu anayependa kueneza matunda ya Uhuru kwa wananchi wote kwa ajili ya manufaa yao na maendeleo ya Taifa kwa jumla.

Miiko ya Uongozi wa CCM kutumia madaraka aliyopewa ama kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo, au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume cha lengo lililokusudiwa madaraka hayo. Pia hatakiwi kupokea mapato ya kificho, kutoa au kupokea rushwa, kushiriki katika mambo yoyote ya magendo au mambo mengine yaliyo kinyume cha lengo lililokusudiwa madaraka hayo.

Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa ndicho Kikao Kikuu cha CCM kupita vyote na ndicho kitakachokuwa na madaraka ya mwisho. Kutunga au kubadilisha sehemu yoyote ya Katiba ya Chama. Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Chama, na uteuzi wa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumthibitisha Mgombea Urais wa Zanzibar.

Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM ni Kupanga Siasa ya CCM na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za CCM; Kupokea na kufikiria taarifa ya kazi za CCM iliyotolewa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa na kutoa maelekezo ya mipango na utekelezaji wa Siasa ya CCM kwa kipindi kijacho.

Pia kuthibitisha, kubadili, kukataa au kuvunja uamuzi wowote uliotolewa na kikao chochote cha chini yake au na kiongozi yeyote wa CCM.

Kazi nyingine ni kubadili sehemu yoyote ya Katiba ya CCM kwa uamuzi wa theluthi mbili za Wajumbe walio na haki ya kupiga kura kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili kutoka Zanzibar.

Wakati wa uchaguzi, kazi za Mkutano Mkuu ni kuwachagua Mwenyekiti wa CCM na Makamu wa Mwenyekiti wa CCM. Kuchagua jina moja la Mwanachama atakayesimama katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Hivyo, Mkutano Mkuu wa CCM, una mamlaka ya kufanya jambo lolote, liwe limefuata utaratibu au laa, na uamuzi wa Mkutano Mkuu wa CCM ni uamuzi wa mwisho, kwa kimombo wanauita 'final and conclusive'.

Sambamba na nguvu hii kubwa ya CCM ambayo ni watu, wanachama wake waliotapakaa Tanzania nzima, mtaji mkubwa wa ushindi wa CCM, ni watu, Watanzania, wanaochagua CCM mwaka hadi mwaka kwenye uchaguzi wa Tanzania ambao ni uchaguzi huru na wa haki. Hili jambo limekuwa likifanyika miaka yote, hivyo na mwaka huu, kazi inaendelea.

**Paskali**
**+255 754 270403**

KONA YA AFYA

# Fahamu kwa undani kuhusu maambukizi ya VVU



Na Dk. Mabula Budodi

KUANZA janga la maambukizi ya UKIMWI miaka ya 1980, kupitia Shirika la Afya Duniani (WHO) inaonesha kuna watu mamilioni wamepata maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo (VVU). Kati ya hao, watu milioni 42.3 wamefariki dunia kutokana na maambukizi ya ugonjwa huo.

Kwa sasa duniani, inakadiriwa kuwa takribani watu milioni 39.9 wanaishi na VVU hadi mwisho wa mwaka 2023.

Pia kupitia WHO inaonesha asilimia 0.6 ya maambukizi haya yanatokea kwa watu wenye umri wa miaka 15 mpaka 49. Katika utafiti huo inaonesha kuwa maambukizi hayo yanatokea zaidi katika nchi za Afrika zaidi katika ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara. Mtu mmoja kati ya 30 ana maambukizi ya VVU.

Kwa mujibu wa WHO, inaonesha kuwa nchini Tanzania, karibu watu milioni 1. 54 milioni wanaishi na maambukizi ya VVU na kati ya hao, idadi kubwa ni kwa wanawake ambayo ni kama asilimia 5.6 wanaume ni asilimia tatu.

Shukurani za dhati ziende kwa serikali kupitia Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anapambana usiku na mchana kuhakikisha sekta ya afya inakuwa na bajeti ya kutosha kupitia misaada na fedha za ndani kukabiliana na tatizo hilo.

Suala hili ni endelevu na mapambano hayana budi kuendelea bila kuchoka. Watoto wanaingia kwenye uhusiano katika umri mdogo wakiwa hawana elimu ya kutosha kuhusu magonjwa ya zinaa na elimu ya uhusiano kwa ujumla.

Katika maeneo ya shule, majarida kama ya FEMA yaliyokuwa yakisaidia kupeleka elimu zaidi kwa watoto kwa mfumo wa picha za kuchora kwa sasa yamekuwa hayaonekani tena.

Elimu ya darasani kuhusu maambukizi ya VVU na UKIMWI imekuwa ikitolewa lakini bado haitoshi ipasavyo kuelezea janga hili kubwa lililosahaulika midomoni kwa watu tena hivyo kufanya kuonekana kama jambo la kawaida.

Na kutokana na misaada ya kupambana na kuzuia maambukizi ya UKIMWI kutoka nchi kama Marekani kutia saini kusitisha misaada zaidi ya kupambana na janga hili, inakuwa kama jambo linalotukumbusha kujifunika shuka huku baridi kali ikiwa inavuma chini kwa chini kwa muda mrefu.

**CHANZO NI NINI?**

Nchini Tanzania, chanzo cha maambukizi ya UKIMWI ni aina ya kwanza ya HIV -1, A,C,D na si HIV- 2 mpaka kufikia mwaka 2018.

Kusambaa kwa maambukizi ya UKIMWI kunaweza kusababishwa na mtu anapofanya ngono bila kinga na mtu mwenye maambukizi au pale damu yake inapochanganyika na damu ya mtu mwenye maambukizi hasa zaidi anapokuwa na vidonda na michubuko katika mwili wake. Pia maambukizi hayo husambaa wakati wa kujifungua kwa maana ya maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto au wakati wa kunyonyesha.

Karibu asilimia 90 ya maambukizi ya UKIMWI kusini mwa jangwa la Sahara yameonekana kupatikana katika kufanya mapenzi bila kujilinda. Pia vitu kama mate, jasho, matapishi, kamasi, mkojo na hata kinyesi vinaweza kuwa mkondo wa kusababisha maambukizi kwa mtu. Pale pale vinapokuwa na damu, uwezekano huongezeka maradufu.

**DALILI ZAKE**

Dalili za watu wenye maambukizi ya UKIMWI, mara nyingi watu wenye maambukizi mapya si rahisi kutambulika au kujifahamu. Huweza kuanza kupata homa ndogo ndogo na mafua, mwili kuchoka, kuvimba kwa mtoki, koo kukereketa, vipele na hata viungo vya mikono, miguu, magoti kuuma pale tu anapopata maambukizi ambayo hukaa kwa wiki kadhaa na kupotea.

Katika muda huu, maambukizi huendelea kusambaa mwili mzima kwenye sehemu tofauti tofauti kupitia walinzi wa awali wa mwili.

Pia hufuatiwa wakati wa maambukizi ambao hauna dalili za kusumbua au kuumwa kama kuvimba kwa mtoki mwilini bila maumivu katika utoki lakini sehemu zote za mwili yaani kwenye makwapa, sehemu za siri, shingoni na kadhalika. Huu muda ndio virusi husambaa kwa kasi zaidi.

Hatua hii ya maambukizi huweza kuchukua miaka minane hadi 10 bila kuona dalili za kusumbua mwili. Hiyo huwa tofauti kwa watoto na wazee ambao huweza kuona dalili mapema zaidi za kusumbua mwili.

Baada ya hatua hii ndio mtu hupata maambukizi yanayokuja na dalili pale mwili unaposhindwa kupambana na virusi hivi na kusababisha homa, kikohozi, kifua kikuu, kupungua uzito, utando wa mdomoni na kadhalika.

Hatua hii kwa watu waliochelewa kutumia dawa huweza kuingia kwenye hatua mbaya zaidi hasa pale kinga mwili inaposhuka zaidi na kufanya mwili kushindwa kupambana kabisa na hata kuishia kupata saratani mbalimbali.

**HADITHI**

Mtaani vijana wamekuwa na uelewa tofauti kuhusu maambukizi ya UKIMWI kwa kumwamini mtu wanapompima papo kwa papo na kumkuta hana maambukizi kisha kufanya naye mapenzi bila kujikinga. Si sahihi kabisa maana kama ilivyoonekana awali.

Mtu anaweza kuwa na maambukizi mapya na akaweza kuambukiza bila kuonekana awali katika kipimo ndiyo maana inashauriwa kurudia kupima tena baada ya miezi mitatu kuhakikisha kama alikuwa hana maambukizi mapya.

Mtu kutambua kujua afya yake mapema kutasaidia kujikinga na kuanza matibabu mapema ili kuishi kwa muda mrefu na kuzuia madhara yanayoweza kusababishwa na maambukizi ya UKIMWI.

Ni vyema kwenda kituo cha afya kilicho karibu au hospitali kwa ajili ya kupima afya na kujikinga kwa ajili yake, mwenza wake na familia yake kwa ujumla. Wahenga wanasema kumjua adui yako mapema ni rahisi kupambana naye.

RIPOTI YA UCHUNGUZI- 3

# Huu ndio mwarobaini mujarabu wa kukabiliana na rushwa barabarani

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** KIGOMA




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, wakiwa kazini. **PICHA: MAKTABA**

RIPOTI ya uchunguzi iliyopita iliweka wazi kilicho nyuma ya pazia kukithiri kwa vitendo vya rushwa kwa askari wa usalama barabarabari, si tu mkoani Kigoma bali maeneo yote nchini.

Katika sehemu hii ya mwisho, ripoti hii inaweka wazi mwarobaini wa kudhibiti moja kwa moja tatizo hilo.

Baadhi ya wadau waiomba serikali kupitia bunge kuifumua sheria ya rushwa na kuipa meno zaidi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika kuhakikisha hawaishii tu kubaini na kuripoti bali kufikisha kwenye vyombo vya sheria matukio ya rushwa.

Pia wametaka makosa ya rushwa kusimama kama jinai tofauti na sasa ambako yamekuwa hayapewi nguvu, hivyo kuwapa kiburi wapokea rushwa. Pia wameshauri kuwekwa kwa kamera barabarani na maeneo fiche ili serikali kujipatia ushahidi pale vinafanyika vitendo vya rushwa.

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007 ilianzisha TAKUKURU kama chombo maalum chenye mamlaka ya kutekeleza sheria hiyo chini ya Mkurugenzi Mkuu ambaye anateuliwa na Rais.

Chombo hiki kimepewa majukumu kadhaa kama vile kuchunguza na kupeleleza tuhuma mbalimbali za rushwa, kuendesha mashtaka ya rushwa dhidi ya watuhumiwa wa rushwa, kupokea malalamiko na kuchunguza malalamiko yanayohusiana na makosa ya rushwa lakini baadhi ya mashtaka yanatakiwa kupata kibali kutoka kwa Mwendasha Mashtaka Mkuu wa Serikali.

Mara kadhaa, vitendo vya rushwa hasa za askari wa usalama barabarani uchukuliwaji wake wa hatua umeonekana kukosa meno hali inayosababisha kuendelea kukithiri na kuibuka kila uchao.

Peter Bwenga, Mfuatiliaji wa masuala ya sheria, anasema kuna haja ya serikali kufanya maboresho muhimu katika sheria zinazotumika kutafsiri makosa ya rushwa na ufisadi.

Bwenga anasema miongoni mwa mambo ya kuyafanyia kazi ni pamoja na adhabu kali badala ya faini ndogo, mtuhumiwa wa rushwa alazimishwe kurudisha fedha zote alizopata kwa njia haramu pamoja na kifungo kisichopungua miaka 10. Pia anashauri makosa ya rushwa kuwa jinai ambako kesi na adhabu zake ziwe sawa na makosa mengine ya jinai kama ujambazi au mauaji.

Mkazi wa Kigoma, Nkana Amiri, anashauri itumike teknolojia katika kuzuia rushwa ikiwamo kuweka kamera barabarani ambazo zitatumika kurekodi matukio yote wanayoyafanya askari kwa siku nzima na kuwekewa mfumo wa ufuatiliaji wa malipo. Anasema teknolojia hizo zinaweza kuwa silaha muhimu katika vita dhidi ya rushwa anayoitaja kuota mbawa huku akidokeza kuwapo kwa elimu ya uzalendo ya kupinga rushwa itakayofundishwa kwa watoto toka elimu ya awali.

Ibrahim Sadick, Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma wa TAKUKURU Mkoa wa Kigoma, anasema kutatua tatizo la rushwa bado ni changamoto lakini wanaendelea kutoa elimu kama nguzo muhimu badala ya matumizi ya nguvu.

Anafafanua kuwa Sheria ya Jeshi la Polisi Huduma Saidizi, Sura ya 332, pamoja na Mwongozo wa Jeshi la Polisi (PGO) ya Julai 2006, zinabainisha wazi makosa ya kinidhamu na hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa askari wanaojihusisha na rushwa.

Anasema TAKUKURU inasisitiza kuwa sheria hizo pamoja na nyingine zinatakiwa zifanyiwe kazi ipasavyo ili kudhibiti mianya ya rushwa barabarani na kwamba wamejiwekea mikakati ya kutoa elimu kwa jamii juu ya ulinzi wa mtoa taarifa ili wananchi wasiogope kutoa taarifa ya vitendo vya rushwa kwa kuwa mtoa taarifa na shahidi anapotoa ushirikiano atalindwa kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizowekwa.

Mpaka sasa, anasema elimu ya ulinzi wa mtoa taarifa imetolewa kwa njia ya vipindi vya redio visivyopugua saba katika redio za kijamii ili kumjengea mtoa taarifa ujasiri wa kutoa taarifa bila woga

Anasema wanatoa elimu kwa Jeshi la Polisi juu ya maadili mahali pa kazi ambayo kwa mwaka 2023 ilitolewa katika wilaya nne na toka Februari 2024 mpaka sasa, imefanyika semina moja katika wilaya zote za Kigoma.

**KAULI ZA WADAU**

Baadhi ya wadau wa masuala ya usalama barabarani wanatoa mapendekezo yao kuhusu kudhibiti vitendo vya rushwa ili kuleta utekelezaji wa haki ya Sheria ya Usalama Barabarani.

Wakili kutoka Msasa Law Chamber Thomas Msasa, anasema viongozi wa Jeshi la Polisi wasimamie askari wanaosimamia utekelezaji wa sheria ya usalama barabarani na wawajenge kuwa rushwa ni jambo la fedheha linalopaswa kufanywa na jeshi hilo.

Pia anashauri faini ya Sh.30,000 ipunguzwe kwa kuwa huenda ni kubwa ndiyo maana madereva wanaona ni heri kutoa 'ushirikiano' kuliko faini ambayo ikiingia serikalini itasaidia kuendesha shughuli za kiserikali.

Wakili Msasa anasema Jeshi la Polisi linapaswa kutimiza wajibu wake wa kukusanya mapato kila mwezi kuliko kuwaacha madereva wa vyombo vya mto kuvunja sheria makusudi kwa kuchukua pesa ya 'ushirikiano' na kuanza kukimbizana kusimamia sheria mwishoni mwa mwaka.

Msasa pia anaiomba TAKUKURU ianze kutekeleza majukumu ya kuwashtaki baadhi ya watu wanaojihusisha na rushwa kama ilivyoanishwa katika marekebisho ya baadhi ya vipengele vya sheria ya kuzuia na kupambana rushwa Oktoba 2024 ambayo inawapa mamlaka ya kushtaki baadhi ya makosa yanayohusiana na rushwa bila kupata kibali kutoka kwa mwendesha mashtaka mkuu.

Bunge lilipitisha muswada wa marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2024 wenye lengo la kudumisha utawala bora na kutokomeza rushwa nchini.

Vifungu viliyofanyiwa marekebisho ni pamoja na kifungu cha 7 kinachoipa TAKUKURU mamlaka ya kuainisha mianya ya rushwa katika taasisi za umma, mashirika ya umma na sekta binafsi, kushirikiana na wadau katika mapambano dhidi ya rushwa, kuhamasisha umma katika mapambano dhidi ya rushwa pia kuipa mamlaka kuzuia na kupambana na rushwa hata chini ya sheria zingine.

Katibu wa KIBOTA, Nuhu Hussein, anapendekeza taasisi zote zinazohusika na usalama barabarani zifuate misingi ya haki, huku akiwataka wakurugenzi wa ofisi za serikali kutumia miongozo, kanuni, na sheria badala ya maamuzi ya kibinafsi.

Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa anayeshughulikia Mipango na Uratibu, Frank Makua, anashauri kufungwa kwa kamera za CCTV barabarani na kwenye stendi za mabasi ili kubaini makosa kwa njia ya uwazi zaidi.

Anasema mfumo wa kamera za CCTV utasaidia kupunguza mianya ya rushwa, kuongeza mapato ya serikali na kuboresha usimamizi wa sheria za barabarani.

**MADEREVA WATAKA CHOMBO**

Madereva nao wanataka kuundwa kwa chombo cha kusimamia na kutetea maslahi ya madereva ni moja kati ya suluhu zilizotolewa na madereva ili kutokomeza tatizo sugu la rushwa kati ya askari wa usalama barabarani na madereva mkoani Kigoma.

Pendekezo hilo lilitolewa na dereva wa mchomoko, Shaban Issa, katika utafiti wa njia za kutokomeza janga hilo. Anasema chombo hicho kitasimama kama daraja kati ya madereva na TAKUKURU ili kuchunguza vitendo hivyo na kutafuta namna ya kuvitokomeza.

"Madereva hatuna chombo cha kututetea kama ilivyo kwa taaluma nyingine ndio maana tunanyanyasika, tunaiomba serikali iunde chombo maalumu kwa ajili ya kutetea maslahi yetu ili kuepukana na uonevu unaoendelea barabarani ikiwemo suala la kumaliza rushwa," anasema.

Ruta Yusuph anasema kuundwa kwa chombo hicho kutasaidia kuweka uwiano wa haki na kuhakikisha kuwa madereva hawanyanyaswi na vyombo vya usalama barabarani.

"Kuna vyombo kama Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambacho kinasimama kupigania haki za walimu, na sisi tukipata chombo chetu ambacho tutakuwa huru kuongea na kikapambana kwa ajili ya maslahi yetu tutamaliza tatizo la rushwa barabarani" anasema Yusuph.

Dereva wa mchomoko, Festo Mlila, anapendekeza kuwa askari wa usalama barabarani waorodheshe makosa na kutoa namba ya malipo ya faini na kwamba hilo litasaidia kuondoa ufanyaji kazi wa mazoea na kuhakikisha kuwa madereva wanakuwa makini na sheria za barabarani.

Viongozi wa madereva wanapendekeza waondolewe askari wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa. kwani tabia hiyo inaambukiza wakitoa mfano wa askari aliyebadilika kutoka kutokupokea rushwa hadi kuwa sehemu ya tatizo na wanasisitiza umuhimu wa hatua kali dhidi ya watumishi wa aina hiyo.

**RPC ASISITIZA TAARIFA**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Filemon Makungu, anasema ni wajibu wa kila mwananchi kutii sheria bila shuruti, kila mtu afanye majukumu yake ili kuepuka kuvunja sheria zilizowekwa.

Anasema wanaendelea vizuri na utekelezaji wa sheria ya usalama barabarani, wanawafundisha wananchi juu ya utii wa sheria bila shuruti licha ya kuwa ukiukwaji wa sheria upo kwa mfano kwenye makosa ya kuendesha vyombo vya moto bila leseni, bima, na mwendo kasi na kwamba wanaendelea kusimamia sheria na wasiotii sheria inachukua mkondo wake.

MAISHA

FEBRUARI 9, 2025
Nipashe


Baba, Mama na ... apili




# Agbada vazi linaloheshimisha

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| P | ■ | T | A | N | G | A |
| A | ■ | ■ | ■ | D | ■ | N |
| N | ■ | B | U | U | ■ | G |
| G | O | A | ■ | G | U | U |
| A | ■ | M | B | U | ■ | K |
| N | ■ | B | ■ | ■ | ■ | I |
| I | B | A | K | I | ■ | A |

## FUMBO TOTO

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

DAI, KAA, ARA, KUU, AMANI, SHIME, ITIKA, DAKWA, PAKWATA, ENGULIA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI


HAYA WATOTO WAZURI, LEO TUPO NA MCHEZO WA NAMBA. TAFUTA VIFUNGU VIFUATVYO VYA NAMBA KATIKA JEDWALI HAPA CHINI. VIFUNGU HIVYO VIPO KUANZIA KUSHOTO KWENDA KULIA NA JUU KWENDA CHINI

**7550 4116 265365 618178 5715**

| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | 7 | 5 | 7 | 8 | 9 | 8 | 0 | 5 | 7 | 8 | 9 | 1 | 2 | 3 | 9 | 3 | 8 | 9 | 1 | 7 |
| 2 | 8 | 9 | 4 | 6 | 1 | 0 | 8 | 7 | 3 | 4 | 6 | 8 | 2 | 3 | 7 | 4 | 9 | 0 | 4 | 3 |
| 8 | 1 | 2 | 3 | 7 | 8 | 9 | 0 | 1 | 9 | 9 | 6 | 5 | 2 | 3 | 6 | 5 | 6 | 4 | 4 | 5 |
| 6 | 4 | 7 | 6 | 4 | 7 | 5 | 6 | 5 | 6 | 7 | 5 | 6 | 1 | 8 | 1 | 7 | 8 | 1 | 9 | 8 |
| 3 | 7 | 2 | 1 | 1 | 1 | 7 | 8 | 2 | 7 | 8 | 3 | 8 | 3 | 4 | 3 | 4 | 9 | 3 | 4 | 7 |
| 9 | 9 | 2 | 1 | 3 | 4 | 8 | 4 | 7 | 5 | 7 | 4 | 6 | 4 | 7 | 3 | 8 | 7 | 1 | 2 | 8 |
| 6 | 7 | 4 | 8 | 9 | 2 | 7 | 8 | 1 | 2 | 5 | 1 | 2 | 1 | 7 | 1 | 6 | 3 | 2 | 3 | 1 |
| 2 | 6 | 5 | 3 | 6 | 5 | 3 | 6 | 6 | 7 | 7 | 1 | 8 | 8 | 1 | 9 | 8 | 3 | 2 | 4 | 7 |
| 1 | 2 | 0 | 9 | 1 | 2 | 8 | 1 | 2 | 2 | 3 | 6 | 3 | 6 | 7 | 3 | 3 | 4 | 6 | 4 | 5 |
| 6 | 2 | 3 | 1 | 6 | 3 | 6 | 2 | 3 | 5 | 6 | 2 | 9 | 8 | 1 | 1 | 4 | 5 | 2 | 3 | 5 |
| 2 | 8 | 9 | 3 | 4 | 5 | 2 | 3 | 7 | 3 | 1 | 9 | 7 | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1 | 9 | 0 |

## PAKA RANGI




Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake "usiku mwema mwanangu"

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao "Pata njozi njema mwanetu"

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia "usiku mwema mpendwa wetu"

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia "Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani"

**SWALI**

Makaa ya mawe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Viashiria uovu nyumba ya baba yako

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada ya wiki iliyopita kuhusu uovu wa nyumba ya baba zetu unavyotesa watu wengi. Yako mambo yanakutokea leo na kukutesa, kumbe yanatokana na uovu wa baba yako uliojificha.

Nikasema kuwa uovu uliojificha unafanya ukatili mkubwa sana wa viwango vya juu kwenye maisha ya watu.

Lakini hicho kilichojificha ni zile nguvu za laana zilizoachiliwa kwenye nyumba za baba zetu. Yamkini wewe ni shuhuda huwa unaona kila mwaka matambiko yanayofanyika kwenye nyumba ya baba yako kutia nguvu ule uovu!

Hebu leo twende zaidi juu ya jambo hili. Mahali popote ambapo yalifanyika mambo haya yafuatayo utagundua hiyo nyumba upo uovu uliojificha.

Kama kwenye familia yako wako watu wa aina hii na walifanya mambo haya yafuatayo, ujue upo uovu umejificha pale. Ambao kama hautashughulika nao utaendelea kuharibu maisha yako daima.

Haijalishi wewe ni nani kwani ile ni sheria inatafuta na kama hujaijua haiwezi kubadilika wala maisha hayawezi kubadilika. (Zaburi 74:20) "Ulitafakari agano; Maana mahali penye giza katika nchi Pamejaa makao ya ukatili".

Mahali penye giza ni mahali ambapo pana dhambi halafu pana uovu umefanyika. Ni nyumba yenye kuabudu miungu ndipo mahali penye giza!

Kama kwenye nyumba au familia ya kwenu kuna watu wanaabudu miungu mpaka sasa na ifikapo kila mwezi wa 12 huenda kuitambikia, kuitolea sadaka au wana desturi ya kuabudu makaburini na kuabudu miungu hadi sasa, hapo panaitwa mahali penye giza.

Na hapo penye giza, pamejaa makao ya ukatili. Na huo ukatili ni yale mambo mabaya, maovu yanayotokea. Kama unatoka kwenye ukoo unaoabudu miungu, hiyo sehemu tayari ina giza.

Hapo giza limetanda na ukatili ndio maana vifo kila mwaka, maisha hayaendi, watu wanakutana na ukatili usio wa kawaida. Kumbe kuna mahali penye giza jambo baya lilifanyika.

Kuna watu wako mjini lakini nyumba ya baba yako kuna vitu vinaendelea. Uko hapa unapambana na maisha lakini kuna nguvu inayofanya kazi kuanzia kwenye nyumba ya baba yako, ukoo wenu.

Na hiyo nguvu inafanya kazi kutokana na kuwepo miungu iliabudiwa na wanaendelea kuitolea sadaka. Ndio maana uharibifu mkubwa utakaokutokea ni ule unaotoka kwenye nyumba ya baba yako.

Andiko la Mungu linasema, "Kama misingi ikiharibika, mwenye hali atafanya nini? (Zab.11:3). Kadiri unavyoendelea kufanya matambiko, kuna madhara yanafuata.

Kama hautafanya jambo la kushughulika na nyumba ya baba yako, ipo nguvu ambayo itakuwa inafanya kazi katika maisha yako. Wewe utabaki unajiuliza, mbona mambo hayaendi, mbona hakuna chochote kinachotokea. Hapana, hii ni nguvu iliyojificha kwenye nyumba ya baba yako.

Kumbuka wewe una damu ya baba yako. Ndio maana ili kujua mtoto ni wa baba yupi, damu ndiyo inayopimwa kitaalamu kujua vinasaba. Kwa hiyo uovu ule ulioanzia kwenye nyumba ya baba yako, upo kwenye damu yako.

Unakuta kuna jambo unalisukuma kulifanya na unaingia kwenye matatizo makubwa, mwisho unajuta unajiuliza ni kitu gani? Kumbe ni ule uovu unatembea kwenye damu ya baba yako.

Mfano, kwenye maandiko ya Mungu inatajwa baraka za Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Lakini ukirudi utagundua kuna mambo yalikuwa siyo mazuri yaliyokuwa yakitembea kuanzia Ibrahimu, Isaka na Yakobo.

Pamoja na kwamba kulikuwa na mtembeo wa baraka, lakini kulikuwa na mtembeo wa uovu fulani uliokuwa unafanya kazi ukifuata damu.

Utagundua kulikuwa na roho au laana ya kudhulumiwa. Ndio maana ukishaanza kuota kwenye ndoto ni kama vile unafukuzwa, unadhulumiwa hiyo ni nguvu fulani. Unanyang'anywa vitu kwenye ndoto tayari kuna shida.

Ibrahimu alinunua kisima, Isaka alipokichimba chenyewe akanyang'anywa. Yakobo akadhulumiwa mshahara zaidi ya mara kumi wakati anafanya kazi kwa Labani. Ukigundua sintofahamu ya aina hiyo ukafanya maombi ya kukata mawasiliano utatoka kwenye kadhia hiyo.

Bila shaka lipo jambo umejifunza hapo. Wiki ijayo tutaendelea na viashiria zaidi vinavyotesa wengi. Kumbe chimbuko ni ule uovu uliojificha kwenye nyumba ya baba yako.

**Una maoni, kisa cha kimaisha? Ujumbe mfupi 0715268581. Pia namba hii ipo WhatsApp.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Kuna vitu kwenye maisha ni matokeo ya muda

USIKUBALI hali au mazingira magumu ya maisha uliyonayo, yaue ndoto yako.Moja kati ya vitu vigumu kwenye haya maisha ni kujaribu kuwaaminisha watu hauko vile wanavyokujua.

Kuna watu wengi sana wanaumizwa kisaikolojia au kihisia kwa sababu ya kutaka kuwaaminisha watu umejipata katika sehemu fulani ya maisha, ili kuficha makosa ya zamani.

Ushauri wangu ni kwamba usilazimishe wakuamini haraka kama unavyotaka, endelea kuthibitisha kwa vitendo kwamba wewe ni tofauti na wao. Pia kamwe usiendelee kujilaumu kwa mambo ya jana ambayo huna uwezo wa kuyabadilisha kwa sababu wako ambao hawaamini katika uwezo.

Wakiangalia unachotaka na wakipima uwezo wako, wanaona haiwezekani. Kupima ufanisi na usimamizi mzuri, ni muhimu kwa upangaji na usimamizi wenye mafanikio.

Usiogope kutokueleweka wakati unasonga mbele, bali ogopa kueleweka wakati umefubaa, umechoka kimaisha.

Kuna baadhi ya watu, kitu kinachowachelewesha kupiga hatua kimaendeleo na hasa kiuchumi, ni kuendelea kujutia mambo yaliyotokea huko nyuma.

Kuna wakati utalazimika kuwa kimya. Ndiyo, kuna wakati utalazimika kupotea na kutoonekana kama ulivyozoeleka. Hili ndio jambo gumu linalonipa uchungu moyoni.

Kitu chochote kikubwa na chenye thamani unachokitaka kwenye maisha yako, kinahitaji mambo mawili makubwa, imani na mapambano.

Ili uwe bora lazima ujenge uwezo wa kukabiliana na mambo magumu na nyakati ngumu za maisha yako.

Si kila kitu kitatokea kama unavyotaka, kuna vitu kwenye maisha ni matokeo ya muda. Yaishi maono yako, mengine ni kupoteza talanta.

Rafiki yangu, hakuna mtu atakayekuja kwenye maisha yako kukutimizia malengo yako, isipokuwa wewe mwenyewe. Muda unatosha kabisa kutimiza malengo yako, lakini hautoshi kufanya kila kitu kwenye maisha yako.

Kanuni mojawapo ya mafanikio, ambayo unapaswa kuizingatia kama unataka kutoboa katika maisha haya ya sasa ni kuchukua uamuzi mgumu wa kubadili mwenendo wa maisha yako na malengo yako.

Usiruhusu ukafikia hatua, wababaya wako ndio wakawa viongozi wa kupiga makofi kwenye mafanikio yako.

> **"Wakiangalia unachotaka na wakipima uwezo wako, wanaona haiwezekani. Kupima ufanisi na usimamizi mzuri, ni muhimu kwa upangaji na usimamizi wenye mafanikio.**

Narudia tena leo kuisema kwenu kauli hii. Kuota ndoto ya mabadiliko ya maisha yako, sio tuu kuwaza au kutamani kufikia hali fulani bali kuota kwa usahihi ni kutengeneza picha kichwani ya hali unayotaka kufikia, au mambo unayotaka kuyapata.

Mwenyenzi Mungu hawezi kukuacha ukafa bila kutimiza ndoto zako utaona unapita kwenye misukosuko mingi lakini bado unaishi. Wakati mwingine Mungu hutuma malaika waje kukusaidie bila wewe kujua.

Hivi bado unatamani mapato ya aibu? Hasidi ana hila, lakini anacheka na wewe. Ubaya huwa haujifichi.

Majivuno ambayo hayajashughulikiwa, huanza kuunda mtazamo mbaya juu ya maisha, ambao huzingatia hasi badala ya chanya.

Sisi ni wepesi wa kuwahukumu wengine kwa kasoro zao, huku tukipuuza ukweli kwamba sisi pia tuna kasoro. Maisha yetu yanaanza kuingiwa na ushindani, badala ya umoja.

Katika kitabu Thoughts of Gold in Words of Silver, kiburi kinaelezwa kuwa ni uovu wenye kushinda siku zote. Kwa kweli, matokeo ya kiburi mara nyingi, ni kukosa marafiki wa kweli na kinyume cha hilo, ulimwengu hupenda wanyenyekevu.

Sisi wanyenyekevu ambao wana fahari ya kuwa hivyo, bali wanyenyekevu kikweli. Hata maandiko matakatifu katika Biblia yanasema, kiburi cha mtu humletea aibu, yeye ajinyenyekezaye atapata heshima.

Kiburi hutangulia uangamivu na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko. Afadhali kuwa na roho ya unyenyekevu pamoja na maskini, kuliko kiburi.

Katika kitabu cha Ujamaa kilichondikwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Julai 1968, kuhusu azimio la kukubali aina fulani ya maisha, Mwalimu Nyerere amesema katika hali yetu ya sasa ya uchumi, na katika umasikini wetu, azimio la kukubali aina fulani ya maisha, linaweza kuonekana kama jambo la vitabuni tu.

Lakini ukweli ni kwamba, kuna baadhi ya vitendo ambavyo tutakataa kufanya au kuvikubali kila mtu binafsi au taifa zima, hata kama matokeo ya vitendo hivyo vingeleta ongezeko la uchumi na kutafsiri maendeleo kwa kukua.

• ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI



Juma Jux na mkewe Priscilla walivyofurahia mwanzo wa maisha yao ya ndoa.PICHA:MTANDAO

MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# Agbada vazi linaloheshimisha

VAZI la Agbada lina asili ya Afrika Magharibi, lakini kwa sasa limekuwa moja ya chaguo pendwa kwa wanaume wengi sehemu mbalimbali ya bara hilo.

Waafrika wanaopenda kwenda kitamaduni zaidi huvaa nguo za kudarizi na zenye pande tofauti za vitambaa vya rangi za kupendeza.

Agbada inafaa kuvaliwa katika hafla mbalimbali kama vazi rasmi ikiwamo sherehe za harusi, mikutano ya kibiashara na karamu za kiserikali.

Mtindo wa nguo hizi ni pamoja na kudarizi kwa nguo ya juu na suruali inayolingana rangi.

Nguo hizi zimkwa chenye mwili

etengenezwa kitambaa kuwezesha kupumua.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# Jifunze namna ya kutunza kucha zako

KWA kawaida kucha za mikononi na miguuni zinakabiliwa na mazingira magumu kutokana na majukumu ya kazi za kila siku hali inayochangia kuziweka katika mazingira magumu kiafya.

Mbali na kucha kukosa afya, pia huharibika shepu yake ya awali kutokana na shughuli za kila siku katika maisha ya binadamu yeyote, hivyo ni vyema kuzikinga kucha zako na maradhi kwa kuzifanyia usafi kila siku au mara kadhaa kwa wiki ili kuzilinda zaidi.

Ili kuweza kugundua aina ya kucha zako katika kuzipangilia wakati wa kuzifanyia usafi, unapaswa kuwa makini wakati unachagua rangi ya kupaka, kuangalia muonekano wa kucha zako zilivyo ili uweze kupangalia rangi ziweze kuwa na mvuto zaidi.

Ni vyema kwa mtu anayejali afya ya kucha zake kuchukua muda mwingi kufuatilia kucha zake na kuelekeza nguvu zake katika kuhakikisha zinakuwa katika matunzo mazuri na kujitahidi kubuni mtindo ambao unaweza kuwa tofauti na wengine ambao wanapenda kuzifanya kawaida.

Hata hivyo katika kutunza kucha ziwe nzuri, vyakula ambavyo ni mlo kamili ni muhimu sana, vinginevyo utajikuta ukishauriwa na wataalamu kutumia vitamini mbalimbali kama vile vitamini A, vitamini C, Culcium, Folic Asidi, Protini na Vitamini B12.

**Jinsi ya kusafisha kucha**

Wekeza vifaa vizuri vya kisasa vya kutunzia kucha.

Tumia brash ya kucha kwa kusugua chini ya kucha na kuutoa uchafu na kufikia sehemu ngumu ambapo uchafu unajirundika.

Unaweza tumia mswaki ukiwa huna vifaa vya kisasa.

Tumia maji moto na sabuni ya kunawia mikono.

Anza kwa kusugua chini kabisa kwa kushikilia brush chini na sugua kuanzia nyuma kuja mbele pole pole, kisha juu ya kucha fanya hivyo kwa kuzunguka.

Toa rangi kwa kuloweka pamba kwenye 'polish remover' na usugue kwa vidole vyenyewe huna haja ya kuitoa.

Kwa vidole vya afya na nguvu vipumzishe kwa kutumia polish kila baada ya wiki kadhaa.

Loweka kucha na maji kwenye bakuli au sinki, au kifaa cha uwezo wako hata dishi poa, kwa maji ya moto ya uvuguvugu na pitisha sabuni ya kunawia mikono.

Na ni kucha tu usiloweke mkono mzima, kwa dakika tatu, sabuni kwenye maji hufanya mikono kuwa mikavu.

Suuza kwa maji ya bomba ya uvuguvugu au yaliyokuwa kwenye chombo yaani jimwagie, kisha zifute na taulo laini.

Kisha tumia kikatia kucha kukata maana zitakua laini au kifaa cha kuzipunguza kuweka sawa kama hauzikati.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Chai ya maziwa ya viungo

CHAI ya maziwa ni kifungua kinywa ambacho kwa tamaduni zetu tumezoea kunywa kutokana na kuwapo kwa ng'ombe wengi.

Wengi wamezoea kupika chai ya maziwa kwa kuyachemsha maziwa na kuweka majani ya chai na sukari peke yake.

Leo kwenye safu hii, tutaelekezana namna ya kupika chai tamu ya maziwa na yenye viungo vizuri ambayo itakufanya upate hamu ya kuendelea kutumia.

**Mahitaji**

Maziwa nusu lita, maji dafu nusu kikombe kidogo cha chai, sukari vijiko vitatu hadi vinne kama unapendelea sukari.

Mahitaji mengine ni hiliki punje sita, tangawizi iliyopondwa kijiko kidogo cha chai kimoja, mdalasini mzima vipande vitatu, arki vanilla kijiko kidogo cha chai kimoja na majani ya chai kijiko kikubwa.

**Maandalizi**



Mimina maziwa kwenye sufuria, menya tangawizi na twanga hiliki zako vizuri mpaka zisagike na maganda weka pembeni.

**Jinsi ya kupika**

Weka maziwa jikoni na vitu vyote tulivyoandaa pamoja na maganda ya hiliki kasoro majani.

Acha maziwa yachemke kiasi kabla ya kupanda juu na weka majani ya chai.

Acha maziwa yaje juu kama yanataka kufoka ndio uyaepue na mimina chai kwenye chupa kwa kutumia kichujio na kisha weka kwenye kikombe na ufurahie chai yako na unaweza kunywa na kitafunio upendacho kama vile biskuti na keki.

Hakikisha hujazi maji mengi ili chai isiwe nyepesi na majani ya chai weka kiasi ukizidisha chai inaweza kuwa chungu.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Safisha madirisha ya nyumba kuing`arisha

KUSAFISHA madirisha na milango ya kioo nyumbani ni moja ya mambo yanayochangia kung'arisha nyumba.

Unaweza kuifanya mwenyewe au ukatafuta watu wanaoweza kukusaidia hasa kwa wale wanaohofia kuharibu muonekano wake kutokana na kutokuwa na utaalam japo kuwa ni bora zaidi kuifanya mwenyewe.

Hata pale unapoona kwamba kuna ugumu, si vibaya kuutafuta utalaam huo kutoka kwa wazoefu ili kuepuka gharama ambazo unaweza kuzitumia mara kwa mara kwa sababu ikumbukwe kwamba kazi hiyo haifanyiki mara moja.

Njia nyingine pia unaweza kutumia ujanja ukawaita wataalam wa kukusaidia kwa siku moja, halafu na wewe ukatumia fursa hiyo kujifunza kwa kufuatilia kila hatua wanayoifanya katika siku ya kwanza halafu na wewe ukawa unafanya mwenyewe.

Zifuatazo ni hatua za kupitia ili kufanikisha kusafisha maeneo yenye vioo yang'ae;-

Kwanza kabisa, unatakiwa kupanga muda wa kusafisha ambao jua halipigi moja kwa moja kwenye kioo.

Hiyo ni kwa sababu jua kali linakausha mapema mara unapoanza kuliloanisha kabla ya kuanza kusafisha au kulisuuza na pia inaacha ukungu wa dawa ya kusafishia au matone ya maji na hivyo kukulazimu kurudia tena kazi hiyo.

Ili kuepuka hali hiyo, ni vema usafi huo ukafanyika asubuhi na mapema kabla jua halijawa kali, jioni au kusubiri hadi siku yenye mawingu.

Kabla ya kuanza usafi huo unapaswa kuandaa vitendea kazi vya kusafishia ikiwamo dawa maalum iliyotengenezwa kwa lengo la kusafishia vioo pamoja na maji.





Endapo unatumia maji unatakiwa kuyachanganya na kiasi kidogo cha vinega kwa uwiano wa kipimo kimoja kwa vipimo kumi vya maji.

Vifaa vingine unavyopaswa kuandaa ni sponji, kitambaa kikavu cha pamba au magazeti, brashi ndogo laini na ngazi ndogo endapo madirisha yako yana umbali mkubwa toka ardhini.

Baada ya hapo unaweza kuanza kusafisha kuanzia juu kushuka chini ili usafishe eneo lenye kioo litakate na kung'aa zaidi.

Kufanya hivyo kutakuhakikishia kuwa hakuna uchafu utakaodondokea kwenye sehemu ambayo umeshasafisha tayari. Kama eneo la kioo unalotaka kusafisha ni chafu sana kwa mfano kuna vumbi jingi au utando wa buibui, inakupasa kutumia kitambaa kikavu kuondoa uchafu huo kwanza.

Katika sehemu za kona huwa kuna kawaida ya uchafu kuzama, hivyo unatakiwa kutumia brashi laini kuuondoa.

Loanisha kioo kwa kutumia sponji lenye maji huku ukiepuka kuweka maji mengi kiasi cha kuchuruzikia kwenye fremu ya mlango au dirisha la kioo unalosafisha.

Suuza na kausha kioo kwa kutumia kitambaa kikavu, na mwishoni ng'arisha kwa kufuta na kipande cha gazeti.

Endapo unatumia dawa za kusafishia kioo basi inakupasa kuipulizia kidogo kidogo katika kioo moja kwa moja huku ukifuta haraka haraka kabla haijakaukia.

Tumia gazeti au kitambaa cha pamba ambacho hakitoi nyuzinyuzi.

Kuwa makini kama fremu ya eneo la kioo unalosafisha limetengenezwa kwa mbao, puliza dawa kidogo kidogo na epuka kuigusisha na fremu.

Safisha fremu na kona kwa kitambaa haijalishi ni ngumu kiasi gani unaweza kuondoa uchafu kwenye eneo la kioo lile la kona na fremu kwa sababu ndio linabeba uchafu mwingi zaidi kama huna vifaa sahihi.

Safisha maeneo hayo kwa kutumia kitambaa au fulana ya pamba kwa sababu itanyonya uchafu wote na kuacha fremu safi.

Madirisha ya kioo yanapaswa yawe yanasafishwa kwa kina angalau mara moja kila mwezi au walau kila baada ya miezi miwili.

# Tumia vyema ukuta wako wa jikoni, stoo

Na Restuta James

LEO nitaongelea namna unavyoweza kutumia ukuta wa jiko na stoo yako, kupunguza msongomano wa vitu kwenye maeneo haya muhimu.

Moja ya kazi kubwa ya ukuta ni kuweka kabati la vyombo vyako kama sahani, bakuli, vikombe, visu, pamoja na vifaa vingine vya jikoni.

Kadhalika, stoo kunawekwa mpangilio wa kabati au shelvu linalohifadhi vyakula kama unga, mchele, maharage, ngano, mafuta na vinginevyo.

Kama umefanikiwa kupanga vitu vyote na vikatosheleza kwenye eneo ulilooandaa, ni jambo bora kabisa, lakini kama jiko lako ni dogo na pengine huna sehemu ya kuweka kabati, basi fuatana nami katika makala haya.

Wataalamu wa mapambo wanaeleza kuwa ukuta unaweza kutumika kwa kuweka ubao au shelvu inayoweza kuhifadhi vitu vinavyotumika mara kwa mara jikoni, kama viungo vya chakula.

Unaweza kutengeneza sehemu maalumu ya kuwekea viungo vikopo vyako kama chumvi, mdalasini, hiliki, tangawizi, kitunguu saumu, vya mchuzi, pilau na vinginevyo.


"Ukiviweka ukutani kama inavyoonekana pichani, unalifanya jiko lako liwe nadhifu na lenye kuvutia na inakua rahisi kuviona kwa urahisi," anasema Bahati Alexander.

Anasema sio viungo pekee, bali unaweza kutengeneza shelvu kama hizo ukaweka maua mazuri yanayozalisha kiasi kikubwa cha hewa safi ya oksijeni.

Anashauri pia kwamba kwenye sehemu ya kuweka viungo, unaweza pia kuweka ua kama ulimi wa mama mkwe au rosemary ili kuweka uhai kwenye ukuta wako.



# KATUNI



JUKWAANI
KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO -
SMS - 0713 447766
NYIE NYIE YULE 'UARABUNI' HUYU KWA 'NKAPA' ACHA NCHEKE
KAMA NILIWEKA NADHILI SIHAMI MJINI, ACHA IKANIDHULU
UKATA
KIJIJINI
NAKUONGEZA "SIKU MBILI" UKIFELI NAITIA "SOKONI"
HIVI NILIVYO "KUFAULU" LABDA BWANA ARUDI!
MKOPAJI
"BONDI" NYUMBA
ACHA KUJI-BALAGUZA HAKUNA WA KUKUKOPA
KAMA NDIO GIA "UMEDUNDA" NIMETOKA KUKABWA HAPO KICHOCHORONI!
UNANIKOMALIA NIKURUDISHIE MIA NNE YAKO, KISA GARI IMEHARIBIKA!.. INGEPINDUKA JE?
INGEPINDUKA NINGEKUKWIDA KABLA HATUJA-OKOLEWA.
NISHACHOKA KUKAA BILA KAZI!
AZIMA MIGUU UONDOKE!
BAR
ZAMANI NILIKUWA NIKIPENDA SIHOFII GHARAMA, SHETANI ALIKUWA MKALI
TWENDE AKAKUTANE NA KODI YA NYUMBA ILIYOKWISHA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MTOTO ALIYELALA NA SHIBE UTAMJUA ASUBUHI...

## HABARI KIMATAIFA



Wanajeshi wa Burundi wakielekea uwanja wa mapambano kusaidia jeshi la serikali ya DRC. **PICHA: AFP**

# Jeshi la DRC laapa kuilinda Bukavu, Marekani yatishia vikwazo Rwanda

**Na Moshi Lusonzo**

JESHI la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (FARDC) , limeapa hakuna hata ncha ya eneo litakaloruhusiwa kukaliwa na Rwanda.

Kauli hiyo imetolewa baada ya siku chache waasi wa M23, wanaodhibiti mkoa wa Kivu Kaskazini, kuteua viongozi watakaoongoza eneo hilo.

Hata hivyo, mapambano ya silaha kati ya waasi hao na jeshi la serikali yanaendelea karibu na mji wa Bukavu ulioko Kivu Kusini.

Luteni Jenerali Masunzu Pacifique, kamanda wa kikosi cha tatu cha ulinzi, alisema katika taarifa iliyosomwa na msemaji wake Meja Nestor Mavudisa Mayoyo, kwamba jeshi limejiandaa kuhakikisha usalama wa raia na kuilinda mipaka ya nchi.

"Ziara hii katika eneo zima la mapambano inalenga kufikisha mwisho tetesi zinazoenezwa za uongo kuwa jeshi la Rwanda na washirika wake waasi wa M23 wamelidhibiti eneo hili la kiutawala.

Jeshi liko tayari kikamilifu na linaendelea kuhakikisha usalama wa raia wote bila ubaguzi, pamoja na ulinzi wa mipaka ya nchi." alisema

Alisisitiza "Hakuna hata sentimita moja ya DRC itakayokabidhiwa kwa jeshi la Rwanda na washirika wake kutoka muungano wa AFC na M23,"

Mayoyo alitoa wito kwa wakazi wa jimbo la Kivu Kusini, hususan wa mji wa Bukavu, waendelee kuwa watulivu na wawe na imani na jeshi lao halali la FARDC.

Alihimiza kila raia apuuze taarifa za uongo zinazoenezwa na adui wa nchi hiyo katika mitandao ya kijamii na wasizisambaze katika mfumo wowote ule.

Mayoyo aliwashukuru raia wa Congo kwa kujitolea kwa dhati kwa ajili ya amani na kuliunga mkono jeshi lao kwa njia mbalimbali.

Wakati huo huo, katika mkutano wa baraza la haki za binadamu la Umoja wa Mataifa uliofanyika nchini Uswisi, kamishna mkuu anayeshughulikia masuala ya haki za binadamu Volker Turk alitahadharisha kuhusu uwepo wa unyanyasaji wa kingono unavyozidi kuwa mbaya mashariki mwa Congo.

Alihimiza hatua za haraka zichukuliwe kuepusha mgogoro huo kuendelea kuwa mbaya zaidi.

Congo imeidhinisha tume maalumu ya uchunguzi ya Umoja wa Mataifa kuchunguza madai ya ukiukaji wa haki, huku ikitarajiwa ripoti hiyo itakamilika Septemba mwaka huu.

Katika mkutano huo, Rwanda imekanusha kuhusika na mgogoro huo.

Aidha, Marekani imeonya kuwa itawawekea vikwazo viongozi wa serikali ya Rwanda na DRC kwa kuhusika kwao katika mgogoro wa Congo.

Barua ya kidiplomasia iliyotumwa na Marekani, kwenda Kenya ambayo ni mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ilisema kunahitajika utulivu wa haraka katika eneo hilo na Rwanda kuondoa vikosi vyake ambavyo vina silaha za hali ya juu. "Tunapotoa madai haya ya pande zote mbili, tutazingatia vikwazo dhidi ya wasio na ushirikiano, ikiwa ni pamoja na maofisa wa kijeshi na serikali katika serikali zote mbili," ilisema barua hiyo.

Mwezi Julai, Idara ya Fedha ya Marekani iliweka vikwazo kwa Muungano wa Mto Kongo, muungano wa makundi ya waasi ambao yanajumuisha waasi wa M23.

Baada ya kuiteka Goma, mji mkubwa zaidi mashariki mwa Kongo, wiki iliyopita, Jumatano ilichukua mji mwingine wa uchimbaji madini katika kuelekea mji mkuu wa mkoa wa Kivu Kusini, Bukavu, na kukiuka usitishaji mapigano wa upande mmoja waliokuwa wametangaza.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA),ilikadiria kwamba takriban watu 2,800 walikufa katika mapigano katika mji wa Goma.

Mkuu wa haki za binadamu wa Umoja wa Mataifa, Volker Turk aliambia mkutano wa dharura kwamba unyanyasaji wa kingono katika eneo hilo, ikiwa ni pamoja na matukio ya ubakaji na utumwa wa kingono huenda ukaongezeka.

Wakati huo huo, mataifa ya Afrika ya kati yametoa wito wa kuafikiwa makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya DRC na Rwanda.

Viongozi wa mataifa hayo wamelilaani kwa nguvu kundi la M23 na kuwataka wasitishe vita mara moja.

Akizungumza baada ya mkutano wa dharura wa baraza la amani na usalama la Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika ya Kati (ECCAS) yenye nchi 11 wanachama, Rais wa Guinea ya Ikweta, Teodoro Obiang alisema jumuiya hiyo imetaka mapigano yakome mara moja.

Obiang alisema kwa sasa jumuiya yao inakabiliwa na mgogoro mkubwa wa usalama unaoziathiri nchi mbili wanachama,DRC na Rwanda, ambazo zinakabiliwa na vita vilivyosababisha mgogoro wa kutisha wa kibinadamu katika eneo lao.

"Kama mwenyekiti wa muda wa Jumuiya ninatoa wito wa kufanyika kwa mdahalo wenye tija, kuheshimiwa kwa uhuru na mipaka ya mataifa na nazitaka pande husika katika mgogoro huu zioneshe mazingira mazuri ya ushirikiano kuwezesha njia za amani zilizopendekezwa katika mchakato wa Luanda."

Obiang aliongeza kusema kwamba ili kuhakikisha mgogoro huo hauenei katika maeneo mengine, wanatoa wito mapigano yasitishwe mara moja ili kushughulikia vyanzo vya msingi vinavyozuia maelewano kati ya nchi hizo mbili.

Rais huyo wa Guinea ya Ikweta aidha alisema mgogoro wa Congo unawalazimu kuchukua hatua za haraka ili kuzuia athari za mzozo huo kuwa mbaya zaidi kutokana na makabiliano ambayo yanazidisha hali ya kibinadamu kuwa mbaya.

Wakuu hao wa ECCAS walivitaka vikosi vya Rwanda viondoke mara moja kutoka kwa ardhi ya DRC na eneo maalumu litengwe kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kibinadamu.

# Mfumo wa NaPA kuboresha huduma za usafiri

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MFUMO wa kielektroniki wa anwani za makazi (NaPA) ambao una programu tumizi yaani 'application' utasaidia kuboresha huduma za usafiri na usalama wa abiria na madereva.

Kupitia mfumo huo, kwa kutumia simu janja, madereva wanaweza kupakua 'application' hiyo itakayowarahisishia kuwafikia wateja kwa haraka kwa kuwa ni wa utambuzi wa maeneo.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, alisema hayo juzi katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini hapa wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Anwani za Makazi alipozungumza na maofisa usafirishaji wa bodaboda na bajaji wa mkoa wa Dodoma.

Waziri Silaa alisema mfumo huo ulio chini ya wizara yake unatumia simu za kiganjani na abiria wanaweza kuita huduma ya usafiri kwa kuingiza anwani zao za makazi katika mfumo huo na maofisa usafirishaji, maarufu kama madereva, wanaweza kufika moja kwa moja kwenye maeneo yao.

"Anwani za makazi ni muhimu kwa utoaji wa huduma bora za usafiri kwa kuwa husaidia katika upatikanaji wa maeneo kwa urahisi na usahihi. Hata kama ni mgeni na hauifahamu Dodoma, kwa kutumia mfumo huu wa NaPA utaweza kumfikia mteja kwa urahisi," alisisitiza.

Waziri Silaa alitoa rai kwa maafisa usafirishaji kuwa mabalozi wa Mfumo wa kielektroniki wa Anwani za Makazi kwa kuutangaza na kuutumia katika shughuli zao za kila siku ili kuboresha huduma kwa kuwa mfumo huu unatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya usafiri nchini.

Akitoa salamu za maafisa usafirishaji, Mwenyekiti wa Umoja wa Madereva Pikipiki Dodoma (UMAPIDO), Marwa Nyagake, aliishukuru serikali kwa kufanikisha uundaji wa mfumo huo.

Alisema faida za mfumo huo zinaanza kuonekana katika kurahisisha utoaji wa huduma ikiwemo huduma za usafirishaji.

# Bunge laazimia mambo 11 maji na mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeazimia mambo 11 yanayohusu maji na mazingira ikiwamo Wizara ya Maji ikamilishe uchimbaji wa visima vitano kwa kila Jimbo vilivyoahidiwa na Serikali.

Aidha, utiririshaji wa majitaka na taka za viwandani katika Ziwa Victoria umetajwa kusababisha kupungua kwa samaki, kuongezeka kwa viumbe vamizi, kuharibika kwa mifumo ikolojia muhimu ya viumbe hai vya majini na kupungua kwa ubora wa maji.

Akiwasilisha juzi bungeni taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jackson Kiswaga, alisema baadhi ya visima vinavyoendelea kuchimbwa nchini vimekuwa vikikosa maji licha ya kutumia rasilimali nyingi katika uchimbaji huo.

Kiswaga alisema hali hiyo inasababisha hasara na kurudisha nyuma juhudi za kusaidia upatikanaji wa maji kwa maeneo yote nchini na Bunge linaazimia kwa kushirikiana na wadau wa utafiti (Vyuo Vikuu, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania- TPDC), serikali iboreshe utafiti kwenye utafutaji wa maji chini ya ardhi kwa kuwaongezea uwezo Wataalamu wake pamoja na kutumia teknolojia za kisasa katika uchimbaji wa visima.

Alisisitiza Wizara ya Maji ichukue hatua madhubuti zitakazowezesha kukamilika kwa uchimbaji wa visima vitano kwa kila jimbo.

Pia alisema Bunge linaazimia kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaifa itakayoratibu shughuli za uchimbaji wa Mabwawa ya Maji kwa kuzingatia uhitaji wa maji kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

**ZIWA VICTORIA**

Alisema licha ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhusu utiririshaji wa Majitaka na taka za viwandani katika ziwa hilo bado unaendelea kwa baadhi ya maeneo, ikiwamo mto Milongo.

> **"Ofisi ya Makamu wa Rais ichukue hatua za haraka zitakazowezesha udhibiti endelevu wa utiririshaji wa majitaka katika Mto Milongo ulioko jijini Mwanza," alisema.**

Alisema ziwa hilo limeendelea kuathiriwa na shughuli zisizo endelevu za kibinadamu zikiwamo; uvuvi haramu, uharibifu wa maeneo oevu, kilimo kisichozingatia uhifadhi, uchimbaji madini usiokuwa endelevu. Alitaka halmashauri zote zinazozunguka Ziwa Victoria kutekeleza mikakati iliyopo ya udhibiti wa taka katika ziwa hilo kwa kuzingatia ipasavyo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

"Ofisi ya Makamu wa Rais ichukue hatua za haraka zitakazowezesha udhibiti endelevu wa utiririshaji wa majitaka katika Mto Milongo ulioko jijini Mwanza," alisema.

Pia alisema kutokana na majanga yaliyoyakumba maeneo ya Hanang, Kibiti na Rufiji, Bunge linaazimia itungwe Sheria, Kanuni na Miongozo ya uanzishaji wa Mfuko wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi utakaogharamia utekelezaji wa Mipango na mikakati ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi nchini.

Kadhalika, bunge limeazimia serikali iharakishe mchakato wa kupata maeneo makubwa mbali na makazi ya watu kwa kuzingatia Kanuni za Mipango Miji ili kutumika kuhifadhi taka zinazozalishwa katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya jirani.

"Uhifadhi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi upewe kipaumbele katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025- 2050,"alisema.

"Bunge linaazimia kwamba" Serikali iharakishe mchakato wa kutunga Sheria ya usimamizi wa Uchumi wa Buluu kwa kuzingatia Malengo ya Sera mpya ya uchumi wa Buluu ya mwaka 2024,"alisema.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Moyo hauna kifuniko, ungefungua uone unavyokereketa juu yako



**Na Adam Fungamwango**

> **Wimbo huo unaitwa 'Tofiki', ulirekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1980, ukitungwa na Bakari Milanzi. Moja ya maneno yaliyowekwa kwenye wimbo huo, ambayo yaliandikwa ni kwamba laiti moyo wake ungekuwa na kifuniko, angemwita na kumwambia fungua uone unavyokereketa.**

MAPENZI ni kizungumkuti. Ndiyo kitu pekee duniani ambacho hakina 'fomula.' Hakuna kanuni. Hakuna chochote ambacho unaweza kujifunza ukawa bingwa wa mapenzi. Mapenzi ni kitu ambacho hutokea kwa bahati nasibu. Na wakati mwingine huendelea kuishi kwa bahati nasibu hivyo hivyo. Ni kitu ambacho kimewashinda wasomi na maamuma. Kimewasambaratisha matajiri na masikini.

Kila mmoja analia mapenzi. Kwa sababu hakuna mtu anayejua kwa nini amependa, au kupendwa. Je anapendwa kweli au anaigiziwa? Siku zote kwenye mapenzi, leo raha kesho tabu. Msondo Ngoma Music Band, walishawahi kutoa wimbo ulioitwa 'Mpenzi Kizungumkuti.' Moja kati ya maneno yake yanasema wala usishangae kuona mtaani kwenu kuna sherehe, wawili wapendanao wanafunga ndoa. Na hapo hapo jirani tu kuna kijana amejinyonga kwa sababu ya mapenzi.

Ni mapenzi tu ndiyo unaweza kuona tajiri akakataliwa licha ya mali zake zote, na masikini akakubaliwa.

Ni mapenzi tu ndiyo yanaweza kumtoa mtu kwa hiari yake, Oysterbay akikaa kwenye nyumba ya kifahari, na kitanda kama mfalme, kwenda Manzese au Tandale kulala kwenye chumba kimoja, kwenye kitanda cha kamba.

Ukiondoa mapenzi, hakuna kingine kinachoweza kumfanya binadamu kufanya jambo hilo ambalo ukiliangalia sana na ukilitoa kwenye mapenzi, linabaki kuwa la ovyo na kipuuzi tu.

Ndiyo maana hadi leo hakuna mtu anayejua mpenzi aliyenaye anampenda kwa dhati, au kuna kitu kinamfanya ampende. Kwa sababu hakuna mzani wala chochote ambacho kinaweza kuthibitisha hilo. Inabaki ni dhana tu. Lakini moyo wa mtu ni kichaka. Unaweza kumpenda mtu, kumbe yeye anampenda mwingine. Unaweza kupendwa, lakini wewe ukawa humpendi anayekupenda, badala yale unampenda mwingine ambaye wakati mwingine anakusumbua tu, hana habari na wewe.

Dada mmoja aliondokea kumpenda kijana ambaye alionekana hana mpango na yeye. Kijana ilionekana ana mtu mwingine anayempenda. Mwanadada aliumia sana. Akachukua kalamu na karatasi na kumuandikia waraka. Barua hii ikatengenezewa wimbo na bendi ya National Panasonic, iliyokuwa ikimilikiwa na kiwanda cha kutengeneza betri kilichokuwa na makazi yake jijini Dar es Salaam.

Wimbo huo unaitwa 'Tofiki', ulirekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1980, ukitungwa na Bakari Milanzi. Moja ya maneno yaliyowekwa kwenye wimbo huo, ambayo yaliandikwa ni kwamba laiti moyo wake ungekuwa na kifuniko, angemwita na kumwambia fungua uone unavyokereketa. Afungue aone jinsi anavyompenda. Nadhani hiyo ingesababisha agundue jinsi alivyoshiba na mapenzi juu yake, kiasi cha kubadilika na kutotaka kwenda kwa mwingine yoyote. Lakini haiko hivyo, moyo hauna kifuniko, hauwezi kuona wingi wa mahaba aliyonayo moyoni mwake, kilichobaki sasa anauguza vidonda vya moyoni. Wimbo huo uko hivi.

"Tofiki kaka bado ninakupenda, lakini kaka hatuaminiani, wanishangaza sana nashindwa kaka. Watu hufanya ubahili katika mapesa, si katika mapenzi, mbona umeadimika, yapata wiki ya pili, nifanye nini kaka.

Ni nani ajuaye kipendacho moyo? Imani hukutoka. Si usiku wala mchana wewe uko mikondoni mama, subira huwa huna wajitosa, hata ukiathiriwa, wewe hujali hata.

Laiti moyo ungekuwa na kifuniko radhi kukwambia, fungua uone unavyokereketa kaka, lakini sasa imekuwa bure kaka, lakini nauguza vidonda vya moyoni, eeee, ninene nini utambue nakupenda.

Nikiuliza kama kuna kosa, au kitu nilichokosea, husema hakuna kaka oo, kaka ooo.

Moyo ukipenda inakuwa vigumu, kuuzuia inakuwa karaha, kwa mtu ajuaye kitu mapenzi, hiyo wazi naeleza ndugu yangu unisikie." Hayo ndiyo mapenzi 'yana-run dunia.'

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-21

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MARA mbili watekaji wameshindwa kunaswa na polisi kwa sababu taarifa zilikuwa zinapelekwa na Dora, mama mzazi wa mtekwaji.

Ndiyo maana hata pesa ziliendа kuwekwa, watekaji walikuwa wakimpigia simu baba mzazi wa mtoto kuwa wamegundua kuwa kuna mtego na kumtaka arudi na pesa zake. Ni zile ambazo polisi walikuwa wanazotoa kama mtego." Kila alipokuwa akiendelea ndiyo kisa hicho kulivutia watu wengi waliokuwa ndani ya ukumbi huo, na kuwaogopesha wengine.

"Nakumbuka mara ya kwanza mtego uliwekwa maeneo ya Bonde la Kinondoni Mkwajuni, lakini Macky akirejea na pesa alizopewa na jeshi la polisi, na ya pili ilikuwa ni kwenye daraja lililopo barabara ya Kawawa, kwenye kibonde kidogo kati ya Magomeni Mikumi na kwenye 'raundi abauti' ya barabara ya Kigogo. Mitego yote ilifeli. Jeshi la Polisi, kupitia wewe Mkuu wa Kituo Kanda ya Kinondoni, ukaanza kushuku kuwa huenda baadhi ya askari wako wanashirikiana na watekaji kuvujisha siri ili wasikamatwe.

Awali aliyehisiwa alikuwa ni Mwalimu Mkuu wa shule ya Tom Academy, ambayo mtoto Macaire alikuwa akisoma, Dickson Kisanga kuwa huenda anaweza kuwa alishirikiana na watekaji na akawa anavujisha siri. Hakushirikishwa mpango wa pili wa kupeleka pesa, lakini hali ikawa ile ile.

Nadhani baada ya pale ndipo kamanda uliponikabidhi kazi hi kwa sababu kulikuwa na utata mkubwa kuhusu watekaji ambao walionekana kufahamu kila kitu kinachoendelea na kinachofanywa kwenye mpango huu. Macky ndiye aliyekuwa akipata vitisho.

Alikuwa hajui kumbe mzazi mwenzake ndiyo aliyekuwa anawaambia kila kitu watekaji, akiwemo mpenzi wake Malik. Kwa nini walifanya hivi, sisi hatujui, watakuja kutumbia wenyewe. Malik yupo hapa na Dora yupo hapa. Jana nilituma askari wamkamate baada ya kukamilisha ushahidi wote."

Kila mmoja alikuwa kimya. Ni Eddy tu ndiye alikuwa akisisika. Baadhi waliona kama ni mkasa wa kushangaza, wengine wakiona tayari wameshabainika.

"Sasa nitaeleza ni mtego gani ambao niliutega mpaka nikagundua Dora anahusika kumteka mtoto wake mwenyewe." Eddy akanyamaza kidogo akiwaangalia waliohudhuria ukumbini, wengine wakiwa wameimana kwa mshangao, wengine kwa aibu.

**"Sasa nitaeleza ni mtego gani ambao niliutega mpaka nikagundua Dora anahusika kumteka mtoto wake mwenyewe." Eddy akanyamaza kidogo akiwaangalia waliohudhuria ukumbini, wengine wakiwa wameimana kwa mshangao, wengine kwa aibu.**




"Nilianza kufanyia uchunguzi wazazi hawa wote wawili ili kujua kama kuna mmoja anaweza kuwa anatoa siri. Kwa sababu kama zilikuwa zinatoka, basi kuna mmoja kati ya pande tatu, polisi, baba au mama. Na huko polisi ni nani? Lakini kwanza nilitaka kuanza na wazazi. Ndipo nilipohitaji majina yao na namba zao za simu kutoka polisi.

Nilijifanya mimi ni mwandishi wa habari ili wasinihofie na wanipe ushirikiano wao. Kikubwa zaidi niliwaahidi kuwafanyia mpango wa kuwapa pesa kiasi cha shilingi milioni 15 ambacho kinatakiwa na watekaji. Kwanza kabisa nilichofanya ni kuongea nao mmoja mmoja bila mwingine kujua kama ninafahamiana na mzazi mwenzake.

Nilianza na Macky, ambaye niliongea naye, na maongezoi yetu baadhi niliyarekodi kwenye kinasa sauti nikimwambia azma yangu ya kumkopesha pesa ili akawape watekaji wamuachie mtoto."

Eddy alifungilia kinasa sauti ambacho kianza kutoa sauti za watu wawili, ambao ni Eddy na Macky.

******************************************

"Sikiliza nikwambie Macky. Kuna kitu nataka kukusaidia kuhusu hili! Mimi nataka kukusaidie kukupa Sh. Milioni 15 kwa kuwapa watekaji."Usihofu, nina rafiki yangu ana uwezo mkubwa wa kifedha. Anaweza kutuaidia ili kuondokana na adha ya kuwaambia askari polisi kiasi mpaka baadhi yao ambao si waaminifu wanavujisha siri. Zitakuwa za mkopo! Rafiki yangu huyo hana tatizo! Hukopesha pesa, na tutakosa kiasi cha Sh Milioni 15 na kurejesha kidogo kidogo kwa mwaka mzima. Kama ndugu mtajipanga mnaweza kurudisha kabla hata mwaka. Ila mimi binafsi kabla ya kukuletea hizo pesa nina ushauri. Pesa zikishafika, hakuna kumwambia mzazi mwenzio wala askari polisi.

Iwe siri na mimi na wewe. Tuwapelekee tu wachukue watuachie mtoto, halafu kulipa iwe taratibu hadi mnamaliza." Alizima na kuendelea. "Nadhani mmesikia baadhi ya maongeze yetu, na kweli watekaji walimpigia simu na kumwambia zikawekwe kwenye eneo moja la pembeni ya kiwanda kule Mikwambe, Kigamboni.

Tulipoelewana aliondoka, huku nyuma nikamleta mzazi mwenzake Dora, ambaye hakujua kuwa nimetoka kuongea na mwenzake. Yeye pia maneno yalikuwa kama hayo hayo, lakini kwa sababu ni mtoto wa kike sikutaka kumkatisha tamaa au kumfanya afikirie sana, nilimwambia tu kuwa mimi nimejitolea kutoa shilingi milioni 15 ili mtoto aachiwe.

Alikubali, lakini sasa tatizo lilikuwa moja, hatuwezi kufahamu safari hii watekaji pesa watataka ziwekwe wapi. Mtu pekee ambaye huwasiliana nao na kumpa maelekezo ni Macky tu. Dora akaniambia hilo anaweza kulifanya ili kujua.

Nilishangaa kwa sababu tayari nilishampa onyo Macky asimwambie mtu yoyote hata mzazi mwenzake. Ambacho alikuwa hajui Dora ni kwamba mimi nilikuwa tayari nimeshafahamu ni wapi pesa zilitakiwa kupelekwa, lakini nilijifanya sijui. Sasa nilitaka kuona kama Macky anaweza kukiuka masharti tuliopeana au vipi." Alipomaliza kusema hivyo, alifungua kinasa sauti ambacho kilikuwa na sauti yake siku alipoongea na Dora.

***********************************

"Hizi ni mimi mwenyewe nimeamua kukupa, nitazilipa mwenyewe taratibu. Ninachotaka kufanya ni kwamba tukaweke sehemu ambayo wao wataamua ili mtoto wako apatikane arudi nyumbani. na Hili hatuishirikishi polisi.

Ni kwamba nataka watekaji wachukue pesa ili wamuachie mtoto na si mtego kama wanavyofanya polisi." "Unasema kweli?" "Kweli bibie!" "Mbona nitashukuru sana jamani, mtoto wangu sijamuona siku nyingi." "Enhe sasa tutajuaje kama watekaji hao ni lini watautaka mzigo huo kwa sababu anayepigiwa siku zote na kuamrishwa ni mzazi mwenzako tu?"


"Sasa hapo!" "Sasa tunafanyaje?

"Mimi nina wazo !Simjui huyo mzazi mwenzako na sitaki tumuunganishe kwa hili. Ila unaweza kufanya kazi moja tukafanikiwa." "Kazi gani?" Akauliza huku akitabasamu. "Wewe ni mtoto wa kike. Nikisema hivyo unajua. Yule ni mzazi mwenzako. Unaweza kumshawishi ili kujua siku na wapi hiyo pesa watekaji wanataka iende ikawekwe sawa?" "Nitajaribu." "Ninavyojua mwanamke akitaka jambo lake hakuna anayeweza kumzuia.

Tunachotaka sisi kujua tu lini ni wapi ameambiwa akaweke hizo pesa, halafu uje kwangu ili sisi ndiyo tukaweke hizo pesa kwa sababu yeye siku zote pesa zake ni za mtego wa polisi, sisi tutakwenda kuweka mapema zaidi kuliko yeye ili wazichukue kabla za mtego hazijaja. Nadhani tunaelewana hapa." "Nimekuelewa baba. Nitafanya kila linalowezekana kwa ajili ya mtoto wangu, Macaire." Mazungumzo kati ya Eddy na Dora yalimalizika kwenye kinasa sauti na Eddy akaendelea kuzungumza.

"Nia yangu ni ile ile. Kuwatenganisha. Tayari nilikuwa nimetenganisha pande tatu, askari polisi, Macky na mzazi wenzake Lengo ni lile lile ni kutaka kujua kwa nini siri inatoka? Nani atatoa siri? Pia kuwanasa watuhumiwa.

**Itaendelea Jumapili**



# DAYNA ATAMBULISHA 'BALANCE' KIBABE

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya, Dayna Nyange, ameachia ngoma mpya inayoitwa 'Balance' na kuingia katika orodha ya wasanii maarufu waliofanikiwa kutambulisha nyimbo zao mwanzoni mwa mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe, Dayna amesema wimbo huo ni zawadi tosha kwa mashabiki wake ambao walikuwa na hamu ya kusikia kazi yake mpya.

"Wimbo huu ni maalum kwa mashabiki zangu ambao walikuwa wakitaka niwafurahishe. Ni ngoma nzuri yenye mtindo wa Zouk ambao kila mtu atakuwa na uhuru

# RONZE KUWAFURAHISHA WAPENDANAO

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Ronze, amesema katika msimu wa wapendanao, ameandaa ngoma kali kwa ajili ya mashabiki wake.

Akizungumza na EATV jana, Ronze, amesema wimbo huo unaoitwa 'Miamore' utakuwa maalumu kwa watu wanaofurahia mapenzi.

"Ngoma itakuwa kali kwa ajili ya wapendanao. Unajua ni msimu pendwa watu wanataka kusikiliza nyimbo za mapenzi na mimi nikaona siwezi kuwanyima mashabiki zangu lazima niwaletee kitu kizuri," amesema Ronze.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DELAP ATAKIWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Ipswich Town, Liam Delap mwenye umri wa miaka 21, ikiwa hawataweza kumsajili mshambuliaji wa Sporting na Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 26, au mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye miaka 26, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Galatasaray.(***GiveMeSport***)

### EDERSON KUTUA MAN CITY

MANCHESTER City imedhamiria kuimarisha kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao na wameelekeza macho yao kwa kiungo wa kati wa Atalanta na Brazil, Ederson mwenye umri wa miaka 25. ***(Fichajes)***

### VINICIUS MKATABA MPYA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Vinicius Jr mwenye umri wa miaka 24, yuko kwenye mazungumzo na Real Madrid ili kuongeza mkataba wake katika klabu hiyo, ingawa makubaliano hayajakamilika. ***(Relevo)***

### DORTMUND KUMUUZA GITTENS

KLABU ya Borussia Dortmund huenda ikalazimika kumuuza winga, Jamie Gittens mwenye umri wa miaka 20, ambaye analengwa na Liverpool, Manchester United na Chelsea, ikiwa hawatafuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. (***Caught Offside)***

### DIBLING KWENYE RADA ZA SPURS

KIUNGO wa kati wa Crystal Palace na England, Adam Wharton mwenye umri wa miaka 21 na kiungo wa kati wa Southampton, Tyler Dibling mwenye miaka 18, wanafuatiliwa kwa karibu na Tottenham Hotspur. (***Football Transfers)***

### FELLOWS ATAKIWA TENA EVERTON

KLABU ya Everton itajaribu tena kumsajili mshambuliaji wa West Bromwich Albion mwenye umri wa miaka 21, Tom Fellows msimu wa majira ya joto. (***Football Insider)***

### ANGE KIKAANGONI TOTTENHAM

KLABU ya Tottenham Hotspur itazingatia mustakabali wa Ange Postecoglou kama kocha ikiwa watashindwa kuifunga Aston Villa katika Kombe la FA wikendi hii. ***(NipeSport)***

### BARCELOA HAIKUPOKEA PESA

BARCELONA haikupokea pauni milioni 8.5 kutokana na mauzo ya kiungo wa kati wa Porto, Nico Gonzalez mwenye umri wa miaka 23 kwenda Manchester City kwa sababu klabu hiyo ya Ureno ililipa klabu hiyo ya Katalunya ada ya pauni milioni 2.5 ili kupunguza nusu ya kipengele cha mauzo. ***(ESPN)***

### NEWCASTLE KUJENGA UWANJA MPYA

KLABU ya Newcastle United inategemea kujenga uwanja mpya karibu na St James' Park. ***(Telegraph)***

### ARSENAL YAKOMA NA WILLIAMS

WINGA wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22, ni kipaumbele cha usajili kwa kocha wa Arsenal, Mikel Arteta**.** ***(Football transfer)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAANZA MAZUNGUMZO NA VINÍCIUS JR

## Ni juu ya kuongeza mkataba mpya wakati huu wa sasa ukiwa.....

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imewasiliana na wakala wa Vinícius Júnior ili kuanza mazungumzo kuhusu kuongeza mkataba wake, kwa mujibu wa ESPN.

Mkataba wa sasa wa fowadi huyo wa Brazil utaendelea hadi Juni 2027.

**Kwa kawaida, klabu hiyo ya Hispania huanza tu mazungumzo ya kuongezwa mkataba kwa wachezaji wake wakati wanabakiwa na miaka miwili.**

Madrid imeamua kuanza mazungumzo kwa sababu ya nia inayoendelea kutoka Ligi Kuu ya Saudi Arabia.

Madrid wameifuata timu ya mchezaji huyo na kueleza kuwa wanataka kuanza mazungumzo, kuanzia na masuala ya mishahara.

Kwa mujibu wa chanzo cha ESPN mazungumzo yako katika hatua ya awali na kwamba wawakilishi wa Vinícius bado hawajapokea ofa rasmi.

Chanzo hicho kiliongeza kuwa Vinícius anafurahishwa na mkataba wake uliopo Madrid na hana haraka ya kuharakisha mazungumzo.

Mwezi uliopita, Vinícius alisema anatumaini kusalia Madrid kwa miaka mingi.

"Ni muhimu sana kwangu kufikisha mabao 100 na kuwa sehemu ya historia ya klabu hii," alisema Vinícius akiiambia Real Madrid TV.

"Nikiwa na umri wa miaka 24, na baada ya misimu saba, kuandikisha historia ni jambo muhimu sana kwangu na kwa familia yangu nzima. Natumaini nitaendelea hapa kwa miaka mingi zaidi."

Hapo awali ESPN iliripoti kwamba Vinícius alifuatwa tena na wawakilishi kutoka Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia (PIF), ambao unamiliki klabu nne za Ligi Kuu ya Saudia, huku ofa rasmi kutoka Mashariki ya Kati ikitarajiwa hivi karibuni.

Mkutano mpya kati ya wasimamizi wa Madrid na wakala wa Vinícius umepangwa kufanyika ndani ya wiki mbili wakati timu hiyo itakapomenyana na Manchester City katika hatua ya mchujo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, chanzo kiliiambia ESPN.

Vinícius amefunga mabao 17 katika mashindano yote akiwa na Madrid msimu huu, na kuisaidia kuongoza LaLiga na kufika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa.

## HABARI MICHEZO




# ANTONY: NILIPITIA WAKATI MGUMU SANA

**MADRID,** Hispania

ANTONY amekiri kuwa alipitia "wakati mgumu" Manchester United huku akiacha mlango wazi kwa uhamisho wa kudumu baada ya kutua Real Betis kwa mkopo.

Winga huyo ambaye alisajiliwa kwa pauni milioni 81.3 mwaka 2022, alitolewa kwa mkopo kwenda Betis Januari baada ya kushindwa vibaya ndani ya United, ambao bado wanalipa sehemu ya mshahara wa Antony na wanatarajia kumuona akijenga upya thamani yake ya uhamisho kutoka Old Trafford.

Mambo yalianza vyema kwa Antony, ambaye alitajwa kuwa mchezaji bora wa mechi kwenye mechi yake ya kwanza, ambapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 aliulizwa kuhusu kuhamia Betis msimu wa joto, makubaliano ya mkopo na United hayajumuishi chaguo au jukumu la kununua.

"Ikiwa nitakaa kwa muda mrefu, nitalazimika kuzungumza na rais na kila kitu," alisema Antony akiviambia vyombo vya habari.

"Na kwa sasa, nataka kucheza na kufunga mabao na kutoa pasi za mabao.

"Lazima niisaidie timu, baadaye tunaweza kuzungumza juu ya hilo."

Antony aliendelea kusisitiza ukweli kwamba alichagua kujiunga na Betis juu ya klabu nyingine kwani alihisi wanaweza kumpa jukwaa bora zaidi la kusonga mbele kutoka kwa mapambano yake huko United.

"Ndio, nilikuwa na mapendekezo, lakini Betis alipotokea, nilihisi uhakika moyoni mwangu kuwa hapa," alisema Antony.

"Nina matumaini ya kufikia malengo mengi na mambo 1,000. Najisikia utulivu sana, ninajiamini, nina furaha sana. Najisikia ajabu, sasa natakiwa kufanya kazi kila siku ili kuwa katika ubora wangu na kuichezea timu.

"Nilikuwa na wakati mgumu, lakini tunapaswa kuheshimu mchakato. Wazo langu ni kucheza kila kitu na kuchangia mabao."

# Amorim atia neno ushindi wa United FA

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim amesema bao la ushindi la dakika za mwisho la timu yake dhidi ya Leicester City katika raundi ya nne ya Kombe la FA lilionesha timu hiyo iliamini hadi kipenga cha mwisho, lakini "haikuwa na uhusiano wowote na wakati wa Fergie."


Kwa maana moja, matokeo ya Ijumaa usiku yalileta hisia iliyozoeleka kutoka siku za Sir Alex Ferguson.

Hata hivyo, ni uchezaji hafifu wa kipindi cha kwanza ambao ulivuta hasira ya Amorim.


"Ilitubidi kuamini na kusubiri hadi mwisho lakini mchezo huu hauhusiani na wakati wa Fergie. Nadhani uchezaji, tunapaswa kufanya vizuri zaidi," alisema Amorim akiiambia ITV baada ya mechi.

"Hatukuwa na nguvu mwanzoni, haswa kipindi cha kwanza. Kisha kipindi cha pili tulicheza vizuri zaidi, kwa kasi kidogo, kushinda mipira ya pili. Kisha tukafanikiwa kubadilisha mambo kwa hiyo yalikuwa matokeo mazuri sio utendaji mzuri.

"Kocha ndiye wa kwanza kuwajibika, wakati timu moja haifanyi vizuri, ni kocha lakini tuko hapa kufanya mambo na kuona mchezo, kusoma mchezo na kujaribu kuimarika kwa mchezo unaofuata."



# Cambiaso hakuwa na mpango Man City – Motta




**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Thiago Motta ameionya Manchester City kuwa beki wa kushoto Andrea Cambiaso hakutaka kuhamia uwanja wa Etihad mwezi uliopita.

Baada ya Kyle Walker kuondoka kwenda AC Milan, City waliongeza kasi ya kutafuta mbadala wake na kuelekeza macho yao kwa Cambiaso, ambaye ni beki wa kushoto wa asili lakini pia anacheza upande wa kulia wa safu ya ulinzi.

Ofa ya euro milioni 65 iliripotiwa kuwasili lakini hatimaye haikuambulia kitu, ingawa City wanatarajiwa kurejesha harakati zao za kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 msimu wa majira ya joto.

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wa Cambiaso, Motta alisisitiza kuwa macho yake yapo kwa Juventus kwa wakati huu.

"Nina furaha alibaki na timu kubwa kama Juventus," alisema Motta. "Nadhani siku zote alikuwa na wazo la kubaki."

City walitumia fedha nyingi kwenye safu yao ya ulinzi Januari, wakiwasajili Abdukodir Khusanov na Vitor Reis kwa zaidi ya pauni milioni 60 zikijumlishwa, huku fowadi Omar Marmoush na kiungo wa kati Nico Gonzalez pia wakijiunga na kuchukua matumizi ya City kufikia karibu pauni milioni 180.

Beki wa pembeni anatarajiwa kuwa eneo lao linalofuata la kuongezewa nguvu lakini Juventus wako tayari kusimama kidete dhidi ya Cambiaso ambaye mkataba wake huko Turin utaendelea hadi 2029.

HABARI MICHEZO

# MWAMBUSI: TUNGEKUWA KWENYE KIWANGO, JKT ANGEKULA NYINGI

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mwambusi amesema endapo kikosi chake kingekuwa kwenye kiwango chake cha kawaida, wangeichapa JKT Tanzania mabao mengi zaidi ya hayo waliyoyapata kwenye mchezo wa juzi.

Mwambusi alisema hayo mara baada ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kati ya timu hiyo dhidi ya JKT Tanzania uliochezwa uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, ambapo timu hiyo ilishinda mabao 2-1.

Mwambusi alisema wachezaji wake hawakuwa kwenye kiwango cha kawaida, kilichozoeleka kwa sababu wamekaa muda mrefu bila kucheza huku akibainisha kama wangekuwa kwenye kiwango chao wangeweza kupata ushindi mnono zaidi.

"Niliwaambia wachezaji wangu kuwa mchezo wa leo ni mgumu, kwa sababu hatujacheza muda mrefu, na kweli hata aina ya uchezaji wetu bado haujawa kama ile tuvyozoea, hatukuwa na maandalizi mazuri sana, kama tungekuwa kwenye kile kiwango tulichokuwa nacho kabla hatujaenda mapumziko, tungeweza kupata mabao mengi zaidi," alisema kocha huyo.

Aliisifu JKT Tanzania kuwa ni timu nzuri na imewapa ushindani wa kutosha ambapo sasa wanajipanga kwenye kucheza mchezo mwingine dhidi ya Masujaa FC utakaochezwa kwenye uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, alisema mabeki wake hawakuwa makini na kuruhusu mipira mirefu ya wapinzani wao na mashambulizi ya kushtukiza.

"Hatukuwa makini kwenye ulinzi na kuruhusu mabao, hatukuwa makini na mipira yao mirefu wala mshambulizi ya kushtukiza. Tulianza mechi vizuri kwa kushambulia pembeni, wakaona hilo, wakafunga njia, ikabidi tushambulie kwa kutumia eneo la kati ndiyo tumepata bao hata la kufutia mchozi," alisema.

Mabao ya washindi juzi yalifungwa na Bakari Msimu dakika ya 26 na Maabad Maulid dakika ya 68 huku Lameck Lawi, akijifunga dakika ya 64.

Matokeo hayo yanaifanya Coastal kupanda mpaka nafasi ya sita, ikiwa na pointi 21, ikicheza michezo 17, huku JKT Tanzania ikibakia na pointi zake 19, ikiwa nafasi ya tisa.



Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Profesa Haruni Mapesa (wa tatu kutoka kushoto) akionesha medali aliyokabidhiwa na wanamichezo wa chuo hicho walioshiriki mashindano ya vyuo vikuu yaliyofanyika mkoani Kilimanjaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Straika Singida aanza Ligi Kuu na bao

Na Mwandishi Wetu

STRAIKA mpya wa Singida Black Stars, Jonathan Sowah, aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili, ameanza mechi yake ya kwanza akiwa na timu hiyo kwa kufunga bao moja, akitumia dakika saba tu uwanjani.

Sowah, raia wa Ghana, aliyesajiliwa na timu hiyo akitokea Al Nasr ya Libya, juzi alifunga bao lake la kwanza akicheza mechi ya kwanza kwenye Uwanja wa Liti, Singida wakati timu yake hiyo ikicheza dhidi ya Kagera Sugar na kutoka sare ya mabao 2-2.

Alitumia dakika hizo saba tu kufunga bao la kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, huku lingine likifungwa na Marouf Tchakei kwa mkwaju wa penalti dakika ya 62 huku mabao ya Kagera Sugar yakiwekwa wavuni na Salehe Kambenga, dakika ya 21 na Halifa Hassan dakika ya 59.

Straika huyo anakumbukwa kwa kutakiwa na klabu za Simba na Yanga kwenye usajili wa dirisha kubwa msimu huu, lakini katika hali iliyoshangaza wengi akaibuka akiwa na Singida Black Stars dakika za mwisho wa usajili wa Ligi Kuu.

Straika huyo atakumbukwa na mashabiki wengi wa soka ambao walimuona kwenye mechi za Kombe la Shirikisho, hatua za makundi wakati akichezea klabu ya Medeama ya Ghana iliyokuwa kundi moja ya Yanga.

Yanga ilicheza dhidi ya Medema mwezi Desemba 2023 mechi mbili za nyumbani na ugenini, straika huyo akionekana kuwa kwenye kiwango bora hivyo timu kubwa za Tanzania kuanza kumuwania.

Baada ya mechi ya juzi, Kaimu Kocha Mkuu wa Singida Black Stars, David Ouma, alisema wachezaji wake wameathiriwa na utimamu mwa mwili kiasi kwamba hakuwa kwenye kiwango cha kawaida.

"Kilichoniangusha ni kwamba kwenye mchezo wa leo ni utimamu wa miili ya wachezaji wangu na ugeni wa baadhi ya wachezaji waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo," alisema Ouma.

Kocha wa Kagera Sugar, Melis Medo, alishukuru kwa kupata sare ugenini akisema ni mwanzo mzuri kwa timu yake baada ya kupoteza mabao 4-0 dhidi ya Yanga mechi iliyopita.

"Nawashukuru wachezaji wangu, kupata sare na timu kubwa kama Singida ugenini si jambo jepesi kwa sababu ni moja kati ya timu tishio kwenye Ligi Kuu kwa sasa," alisema.

Singida bado ipo nafasi ya nne kwenye msimamo ikifikisha pointi 34, huku Kagera Sugar nayo ikiwa pale pale, nafasi ya 15, na pointi zake 12.

## Wanafunzi Mwalimu Nyerere wahimizwa kushiriki michezo

Na Mwandishi Wetu

WANAFUNZI wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere cha jijini Dar es Salaam wamehimizwa kushiriki kwenye michezo ili kujenga miili yao na kuwa na utayari kwenye masomo.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Haruni Mapesa kwenye hafla fupi ya kuwapokea na kuwapongeza wanamichezo wa chuo hicho walioshiriki mashindano ya vyuo vikuu mkoani Kilimanjaro.

Profesa Mapesa, alisema wanafunzi wanaoshirki michezo akili zao zinaimarika na kuongeza ufanisi darasani katika masomo mbalimbali.

"Niwaombe wanafunzi, kupanga ratiba zenu vizuri ili kuwa na muda wa kushiriki michezo huku pia mkifanya vizuri darasani katika masomo," alisema Profesa Mapesa.

Aidha, alisema Chuo hicho kitetenga bajeti kwa ajili ya ushiriki wa chuokatika michezo mbalimbali.

"Naomba kwa ajili ya mashindano yajayo, maandalizi yaanze mapema, tutaboresha miundombinu hapa shuleni ili wanafunzi wapate sehemu nzuri za kufanya mazoezi," alisema.

Awali akimkaribisha Mkuu wa Chuo, Naibu Mkuu wa Chuo hicho anayesimamia Taaluma, Utafiti na ushauri wa kitaalam, Profesa Richard Kangalawe, aliwapongeza wanamichezo wa chuo hicho kwa kufanya vizuri katika mashindano hayo.

Katika mashindano hayo, Chuo hicho kiliibuka mshindi wa kitaifa wa mpira wa wavu huku pia wakitoa washindi kwenye riadha mita 100 na 200.

Hafla hiyo ilikuwa maalum kwa ajili ya kuwapongeza na kuwapa zawadi wanamichezo wa chuo hicho.

Michezo
Jumapili Februari 9, 2025
Nipashe



Cambiaso hakuwa na mpango Man City – Motta UK. 22

# Simba ina matumaini ubingwa

## Kocha wake, Fadlu aikataa ofa ya FAR Rabat akitaka......

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba pamoja na kushushwa hadi nafasi ya pili, bado ina matumaini ya kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara huku taarifa zikisema Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids, amekataa kwenda FAR Rabat ya Morocco, akiamua kubaki kwenye mitaa ya Msimbazi.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kutokuwa na wasiwasi baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Fountain Gate, Alhamisi iliyopita, badala yake waendelee kuipa sapoti timu yao kila inapokwenda kucheza, kwani ina ubora w hali ya juu ambao unawapa matumaini ya kurejea tena kileleni hivi karibuni.

"Simba ndiyo timu bora kwa sasa nchini, ukiona inapata matokeo mabovu ujue imefanya makosa mengi ya kujidhuru yenyewe, ukiangalia mechi dhidi ya Yanga ambayo tumepoteza, na hizi sare zote mbili ni makosa yetu wenyewe.

Lakini huo ndiyo mpira, Jumanne tunakwenda kucheza mechi dhidi ya Prisons, wanachama na mashabiki wa Simba sasa tuangalie mechi ijayo tuachane na mchezo huu uliopita.

Tumeshuka, tupo namba mbili kwa sasa, kwa hiyo tuna kazi kubwa ya kufanya ili kurejea kwenye uongozi, niwaambie kuwa wasishtuke, pengo ni la pointi moja tu, kwa ubora tulionao tuna uwezo wa kurejea kwenye uongozi, kwa hili, kazi ndiyo kwanza imeanza," alisema Ahmed.

Kuhusu winga wa timu hiyo, Ladack Chasambi ambaye amekuwa kwenye midomo ya mashabiki wa soka na wachambuzi kutokana na kitendo chake cha kujifunga kwenye mchezo dhidi ya Fountain Gate, aliwataka Wanasimba wote wawe na kijana huyo kwani zipo kampeni zinatengenezwa kutaka kumpoteza.

"Kuhusu Chasambi anatuhitaji zaidi sisi familia yake, hatuna budi kumuunga mkono na kumuweka sawa kisaikolojia, ikumbukwe kosa alilolifanya lina faida kubwa sana kwa wapinzani wetu, sasa hao wameanza kumdhihaki ili wazidi kumpoteza asiwe kwenye ubora wake, tukasirike lakini tusimchukie kijana wetu," alisema.

Wakati hayo yakiendelea, habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa kocha Fadlu amepiga chini ofa ya FAR Rabat, ambayo ilikuwa inamhitaji kwa udi na uvumba.

Vyanzo kutoka ndani ya Simba na vingine kutoka nje ya nchi, vinasema kuwa Fadlu amekataa ofa hiyo kutokana na kuridhishwa na kila kitu ndani ya klabu ya Simba, kuanzia uongozi, wachezaji na mashabiki wake ambao wamemfanya kujiona kuwa na amani na furaha kwenye kibarua chake ndani ya Simba.

"Ushirikiano wake na viongozi, kukubalika kwake na viongozi, wachezaji na mashabiki, vimemfanya kukataa kuondoka kwa sababu ndani ya Simba kwa sasa ni kocha anayeheshimika sana, nadhani uliona hata Bungeni Dodoma hivi karibuni Wabunge walivyomshangilia kwa nguvu na kwa muda mrefu lilipotajwa jina lake, yeye na kikosi chake walipolitembelea," kilisema chanzo.

Kutokana na kukataa ofa hiyo, FAR Rabat sasa wamewageukia makocha wawili, Alexander Santos, aliyetimuliwa hivi karibuni na CS Sfaxien ya Tunisia baada ya kufanya vibaya kwenye Kombe la Shirikisho Afrika ikiwa kwenye Kundi A, pamoja na Simba, au kocha wa zamani wa Wekundu hao wa Msimbazi, Abdelhak Benchikha.



Fadlu

## Yanga kicheko sare ya Simba

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeweka wazi kuwa imefurahia mno sare ambayo watani wao wa jadi Simba walipata Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, mkoani Manyara dhidi ya Fountaina Gate, ikisema imewaongezea nguvu na morali ya kupambana kwa ajili ya kuutetea ubingwa wao.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema jana kuwa, sare hiyo imewafanya sasa kuongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu vizuri zaidi tofauti na awali ambapo walikuwa wakiongoza kwa muda na kushuka nafasi ya pili kila watani zao walipokuwa wakishinda.

"Tumefurahishwa na sare ya Simba, imetuweka kwenye nafasi ya kwanza vizuri. Matokeo yale ya sare kati ya Fountain Gate na Simba yamekuwa na faida ya kukaa nafasi ya kwanza bila utata. Sawa japokuwa tunafurahi, lakini furaha hii ituongezee hamasa kubwa na umakini, sasa kampeni yetu ni kuhakikisha tunabaki kileleni mpaka mwisho, kila mechi sasa inabidi tucheze kama fainali," alisema Kamwe.

Katika mchezo huo, Simba ililazimishwa sare ya bao 1-1 huku Ladack Chasambi akijifunga mwenyewe alipokuwa akimrudishia mpira golikipa wake, Moussa Camara.

Ni matokeo yaliyoifanya Simba kushindwa kukwea tena kileleni na kubakia na pointi 44 kwa michezo 17 iliyocheza, ikiiacha Yanga kileleni ikiwa na pointi 45.

Hata hivyo, pamoja na furaha, Kamwe alitoa angalizo kuwa michezo ya Ligi Kuu bado ni mingi na chochote kinaweza kutokea mbele, hivyo kuwataka wanachama na mashabiki wa Yanga kuungana na kuipa sapoti timu yao.

"Ligi bado mbichi sana, huwezi kusema tumeshakuwa mabingwa, kuna mechi nyingi mbele za kucheza ambapo chochote kinaweza kutokea, ili kuepuka hayo kama taasisi inabidi tuwe imara kuanzia viongozi, benchi la ufundi, wachezaji na mashabiki, wote tuungane ili kuutetea ubingwa wetu wa ligi," alisema.

Kamwe, alisema wanakwenda katika mchezo wa Jumatatu kucheza na JKT Tanzania kwa nguvu zote na tahadhari ya hali ya juu.

"Tutakwenda kucheza kwa nguvu zote na tahadhari ya hali ya juu dhidi ya JKT Tanzania, kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, tunajua mechi itakuwa ngumu kwa sababu tunakwenda kucheza na timu ambayo msimu uliopita tulitoka nayo suluhu kwenye uwanja wao," alisema Kamwe.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >